# Utungu wa Kuzaa

Phoenix, Arizona, USA
Januari 24, 1965

1 Na tuinamishe vichwa vyetu.

Mungu mpenzi, tunashukuru sana leo kwa ajili ya huku kububujika kukuu kwa Uwepo Wako, katikati yetu, ambako kumetokea tayari. Nasi tunatarajia jambo hili, kupita kiasi, kwa wingi sana, alasiri ya leo. Tunakushukuru kwa ajili ya wimbo huu wa ajabu kutoka kwa mwanamke huyu mzuri Mkristo ambaye ndiyo kwanza ameimba wimbo huu; na Roho Wako aliyeshuka, na tafsiri yake. Bwana, jalia iwe hivyo, tunaomba. Na, Mungu, ninaomba ya kwamba utambariki kila mmoja wetu, na jalia mioyo yetu ijazwe na furaha tunapoona jambo hili likitukia.

Mungu mpendwa, tunaomba, alasiri ya leo, kama kuna wengine hapa ambao hawako tayari kukutana na Wewe, jalia hii iwe ndiyo saa watakayofanya uamuzi huo wa mwisho na watakuja Kwako, kupitia Kuzaliwa upya. Tujalie.

Tubariki sote, Bwana, ambao tumekuwa safarini kwa muda mrefu. Tunaomba ya kwamba utatufundisha mambo mapya kwa Neno Lako. Tupe ufahamu bora zaidi kwa Roho Wako, Bwana. Jalia Yeye aje na kulifasiri Neno. Mfasiri pekee tuliye naye ni Roho. Tunaomba ya kwamba Yeye atatujalia hayo, leo. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada fulani anaanza kutoa unabii. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

2 Hiyo inatosha. [Ndugu fulani anazungumza na ndugu mwingine — Mh.] Ni wakati ulioje! Sijui mahali bora zaidi pa kuwa, isipokuwa iwe ni Mbinguni, kwa kuwa tunasikia tu upako wa Huo sasa, mnaona, tukiketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tumekusanyika katika ulimwengu wa Roho.

Mungu ambariki Dada Florence! Naye anapitia katika wakati wa huzuni, na mashaka; baba yake ndiyo kwanza aage dunia. Nami na—naomba, "Mungu, mbariki mtoto huyo."

Na Ndugu Demos, mzigo juu ya mabega yote mawili, na uzito wa mikutano hii yote na kadhalika. Yeye anahitaji maombi yetu, pia. Mungu ambariki Ndugu Shakarian!

Ndugu Carl Williams, hakika nina furaha kuwa hapa katika mkutano huu pamoja nanyi, miongoni mwa ndugu hawa wote wazuri. Nami nilikuwa na majaliwa ya kukutana na wengine. Na sasa hii ndiyo sehemu yangu ya kumalizia ibada, kadiri nijuavyo mimi, kwa hiyo, mbona, ninatarajia sasa kuweza kupeana mikono na baadhi ya watu hawa wazuri, na—na kukutana nao, kwa kuwa ninatarajia kutumia Umilele pamoja nao, katika—katika Nchi bora.

3 Ni—ni kitu kidogo tu, natumaini sitaeleweka vibaya. Na si kwa bahati mbaya, sidhani, kwa kuwa na—nafikiri ilikuwa ni jambo la busara, ya kwamba jana nilipewa zawadi na rafiki yangu hapa, kutoka kwa rafiki yangu, Danny Henry. Alikuwa mvulana … Siku moja, katika mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo huko California, nilikuwa na m—mkutano. Nilikuwa nikizungumza kwa nguvu sana dhidi ya—ya hali ya wakati huo.

Nami na—natumaini ya kwamba kila mtu anaelewa hilo, sina chuki moyoni mwangu. Si hivyo. La. Hakika mtafahamu simaanishi hivyo. Lakini sina budi kusema tu kile kinachonijia kusema.

Na halafu baada ya hayo, maskini jamaa huyu, ndugu wa Kibatisti … Nami nafikiri yeye ni jamaa fulani wa mchezaji fulani wa sinema. Naye akashuka kuja kunikumbatia, kusema, "Bwana akubariki, Ndugu Branham. Ninataka tu kukuombea." Naye akaanza kunena katika Kifaransa. Na mvulana huyo hajui hata neno moja la Kifaransa.

Na mtu fulani akainuka, kwa namna fulani ni mwanamke mkubwa. Kutoka … Ninaamini alitoka Louisiana. Akasema, "Hicho ni Kifaransa."

Ndipo kulikuwa na mtu kule, kasema, "Hicho ni Kifaransa."

Nao walikuwa wameandika ilikuwa ni nini. Nina nakala halisi hapa. Na ndipo, ikawa, kijana mmoja akitembea kutoka nyuma, na akija mbele, anataka kuona maandishi yao. Naye alikuwa mkalimani wa Kifaransa wa Umoja wa Mataifa. "Kifaransa kabisa."

4 Nami ningetaka kusoma maandishi haya. Hiki ndicho kijikaratasi cha asili cha mmoja wao, na kilitoka kwa mtu huyu aliyekuwa amefasiri. Huenda nisiweze kutamka jina lake vizuri kabisa. Le Doux, Victor Le Doux, yeye ni Mfaransa halisi. Sasa, huu hapa ujumbe.

> *Kwa kuwa umechagua njia iliyo nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi, umeenda kwa hiari yako, umechagua uamuzi mzuri na sahihi, na ni Njia Yangu. Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa mno ya Mbingu inakungojea. Ni uamuzi wa fahari jinsi gani umefanya! Jambo hili, lenyewe, ndilo litakalotoa, na kutimiza, ule ushindi mkuu sana katika Upendo wa Kiungu.*

Nilipopata hilo … Mwajua, wakati niliposikia kwa mara ya kwanza watu wakinena kwa lugha, si—nisingekosoa kitu, mnaona, kwa sababu nimeona ni kweli. Lakini, daima nilishangaa. Lakini wakati jambo hilo lilipotukia, na nikijua agizo lilikuwa ni nini, nyuma yake, ni—nilijua lilitoka kwa Mungu.

5 Ndipo, ndugu yake anayeketi hapa, mwanasheria a—anayejulikana sana, akanipa zawadi kutoka kwa Danny. Danny alitoka Nchi Takatifu hivi karibuni. Naye alikuwa amelala juu ya kaburi, kaburini, hasa, mahali Yesu alikuwa amelazwa baada ya mauti Yake. Na alipofanya hivyo, alisema alianza kuniwazia. Na—na Roho wa Bwana akamjia, ndipo akakwea kwenda Mlima Kalvari ambako kule kusulibishwa kulitukia, basi akatwaa kipande cha mwamba. Ndipo akarudi na kunitengenezea jozi ya vifungo vya sijafu kutokana nacho. Nami kwa kweli ninavipenda.

Na sasa, hili, bila shaka, Danny hajui hili. Lakini, asubuhi ya leo, wakati nilipokuwa nikiomba, niliviangalia tu hivyo vifungo vya sijafu, na kila kimoja cha hivyo, kama ukiangalia, kina alama ya damu, na pia kina mstari ulionyoka moja kwa moja ndani ya kila kimoja. Na hapa kwenye ujumbe alioutoa kutoka kwa Mungu, wa njia nyofu, iliyo nyembamba. Jinsi unavyolingana kabisa, vile vile kabisa! Nilifikiri hilo lilikuwa kwa namna fulani labda la kimbinguni. Ama, hakika ninamshukuru Danny. Mwambie, ndugu, jinsi ninavyothamini jambo hilo. Na ninii … Jambo jingine la ajabu, nilimwomba mke wangu asubuhi niliyovaa shati, ilipaswa kuwa na vifungo vya sijafu, naye akasema, "Nilisahau kukuletea sijafu zako," kwa hiyo Bwana alinipa vingine.

6 Loo, ni maisha yenye utukufu! Sivyo, ndugu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kutembea tu katika urahisi wa—wa Injili! Na hata hivyo, katika urahisi Wake, ndilo jambo kuu sana nijualo. Sijui kitu juu Yake. Na kwa kuwa lilifanywa rahisi, hata nikawa na nafasi ya kuingia Kwake, unaona, pia, kwa neema ya Mungu.

7 Sasa, alasiri ya leo, sitaki kuchukua muda mwingi, kwa sababu ninajua mnaenda makanisani usiku wa leo. Nafikiri, ninyi nyote wageni hapa mnapaswa kuangalia kote jukwaani, kuwaona wahudumu hawa, nao ni, loo, watafurahi kuwa nanyi katika ibada yao usiku wa leo. Watakufanyia mema. Hapana shaka uliendа kwenye shule ya Jumapili asubuhi ya leo mjini. Na wakati tukiwa na mikutano hii, na tukiwa Wafanyabiashara wa Injili Yote, nafikiri inatubidi kuyapa makanisa yetu msaada wote tuwezao, kwa kuwa huko ndiko wafanyabiashara wetu huenda. Na, sasa, ni nyumba ya Mungu, nami natumaini mtatembelea kanisa fulani usiku wa leo.

Kesho usiku ndio mwisho wa mkutano, ninaamini, na nadhani wamemtangaza msemaji. Ambapo, nina lengo la kuwa hapa, Bwana akipenda, kusikia ujumbe wake.

Mungu ambariki kila mmoja wenu.

8 Sasa, mimi, sidai kuwa mhubiri. Mimi—mimi kwa namna fulani ninanii … Sina elimu ya kutosha kujiita mhubiri. Mhubiri, unaposema hivyo, wanakutarajia uwe na digrii kadhaa chuoni. Na—nami sina kitu ila kombeo dogo *Hili*. Mnaona? Ninajaribu kuwafuata kondoo wagonjwa, nikiweza, kuwarudisha kwenye malisho ya Baba.

Kama nikifanya makosa, nisameheni. Mimi si mwanatheolojia. Simlaumu mwanatheolojia. Theolo- … Theolojia ni sawa. Ni kile tunachohitaji. Lakini wakati mwingine mimi hukosoa hali ambayo tumeingia. Hilo halimaanishi mtu fulani binafsi. Ni Ujumbe tu. La—laiti isingalikuwa ni mimi wa kuutoa. Linanirarua vipande-vipande, maana mnajua jinsi mnavyojisikia juu ya watoto wenu wenyewe. Mnaona? Je! si unachukia kumkaripia mtoto, kumpigia makelele, ama cho chote kile, hata hivyo? Mimi ni mzazi, pia, nami najua kile inachomaanisha. Nami na—natumaini ya kwamba mnanisamehe.

9 Nami nawatakeni mfanye hivi. Mnapokuwa mnaketi, alasiri ya leo, nitawaomba kibali chenu. Nina maandishi mafupi, machache hapa. Kama nilivyowaambia, sina budi kuandika hili, kuandika Maandiko *yangu*. Ilikuwa kawaida ya kwamba, ningeweza karibu kunukuu Biblia kwa moyo, lakini si sasa. Nilipitia vita vingi sana, nikawa mzee sana kwa hilo. Lakini ninatumaini ya kwamba—ya kwamba mtanisikiliza kwa muda kidogo tu, alasiri ya leo, na kwa kweli fungueni tu moyo wenu na kujaribu kuelewa ninachojaribu kuchimbua. Ndipo nadhani itakuwa ni bora zaidi, hasa wachungaji wa mji na mahali mbalimbali. Na—natumaini ya kwamba mtasikiliza kwa makini sana.

Na sasa mfanye hivyo, fanyeni kama nifanyavyo ninapokula sambusa yangu ninayopenda sana, ya cheri. Baadhi ya nyama ninazopenda sana, ni kuku. Lakini wakati ninapokula kipande kizuri cha sambusa ya cheri na ninakumbana na mbegu, sitaacha kula sambusa hiyo. Ninatupa tu mbegu, na kuendelea kula sambusa. Mnaona? Nikifikia kwenye mfupa wa kuku; siitupi kuku. Ninautupa tu mfupa.

Kwa hiyo, vipi kama ningesema jambo fulani ambalo hamngekubaliana nalo, wakati wowote? Tupa tu sehemu hiyo mbali. Na, lakini, liangalie vizuri sana, hakikisha ni mfupa, sasa. Mnaona? [Kusanyiko linacheka — Mh.] Na halafu pia niseme, kama ni Mbegu, kumbuka, Inaleta Uzima mpya. Kwa hiyo angalieni kwa bidii sana, na Bwana na awabariki.

10 Ndugu Carl Williams alisema jambo fulani hivi majuzi juu ya kuvunja mkutano, kuwaombea wagonjwa,

jambo ambalo lingekuwa ni zuri sana. Ninajua hilo lingekuwa zuri. Lakini tunaninii tu…hatujajiandaa hapa kwa ajili ya jambo hilo, kuleta mstari wa maombi. Nami sijui kama Ndugu Oral, ama ye yote wa hao ndugu wengine wamewahi kuwa na mistari ya maombi kwenye mikutano hii au la. Sijui. Nimejaribu, mara mbili tatu. Lakini, kwa kawaida, kama kundi kama hili, itakubidi kusambaza kadi za maombi, unaona, ili kufanya hivyo. Maana, huwezi. Si uwanja wa michezo. Ni nyumba ya Mungu. Mnaona? Imewekwa wakfu kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunaninii … Wanasongamana na kusukumana. Na unachukua kadi, unawasimamisha kwenye mstari, kwa utaratibu.

Kwa hiyo Billy akaniuliza, kasema, "Je! Niende kule na kutoa kadi? Watu wananiomba kadi za maombi."

Nikasema, "La, Billy. Hebu na tumwache Roho Mtakatifu afanye yale anayotaka kufanya." Mnaona? Hilo, mnaona, na hebu labda ajenge imani, na mponywe papo hapo mahali mlipo. Mnaona? Lakini ninii … Mnaona?

Uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo katika Injili. Wala huwezi kung'angania jambo dogo. Kila mtu anajua jambo hilo. Lakini wao … Ni chambo ambacho hutumika kuwafanya watu kuamini katika Uwepo wa kimbinguni, ama Mungu, wa Kimbinguni yupo. Halafu basi, kwa jambo hilo, kama wanaweza kutambua Uwepo Wake, basi wanaponywa, mnaona, kwa imani, wakiamini jambo Hilo.

11 Sasa nataka kusoma machache kutoka kwenye Neno la Mungu, Agano Jipya. Na halafu nataka kuchukua somo kutoka kwenye Agano hili Jipya, na Andiko hili, na kuzungumza alasiri ya leo juu ya somo kwa—kwa muda kidogo tu. Nami sitaki kuwaweka kwa muda mrefu sana kwa ajili ya ibada usiku wa leo. Lakini kumbukeni, natumaini nimejiweka dhahiri. Lipeni usikivu wenu kwa muda kidogo, tafadhalini.

Sasa, kabla hatujafanya jambo hili, hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena.

Mwajua, tungeweza kuimba sana. Tungeweza kupiga kelele kupita kiasi, hata tukapwelewa na sauti. Nasi tungeweza kuimba wakati usiofaa, ama kupiga kelele kwa wakati usiofaa. Lakini hapa kuna jambo moja, kamwe hatuko nje ya utaratibu tunapoomba. "Ningetaka watu waombe kila mahali, wakiinua mikono mitakatifu, bila shaka." Ama …

12 Baba, ni majaliwa makubwa sana mwanadamu aliyopata kuwa nayo, ilikuwa ni kufunga macho yake na kuufungua moyo wake, na kuzungumza Nawe. Nasi tunajua ya kwamba Wewe unasikia, kama tungeweza tu kuamini ya kwamba Wewe unasikia. Kwa kuwa Yesu alisema, "Mkimwomba Baba neno lo lote katika Jina Langu, mtapewa." Hiyo ilikuwa kwa masharti, kama tusingelitilia shaka. Kwa hiyo, Baba, tusaidie kuamini, alasiri ya leo, ya kwamba maombi yetu tutapewa. Na jalia kusiwe na shaka hata moja, po pote. Lakini jalia litimie, mambo tunayoomba. Na hiyo ni kusema, Mungu, kwa ajili ya kuliheshimu Jina Lako kuu leo, kwa kuingiza katika Ufalme Wako kila mtu aliyepotea na kila anayetangatanga aliye chini ya sauti yetu, ama pale ambapo kanda hii itawahi kufika, huko kwenye nchi za makafiri, mahali ambako zitaenda kote ulimwenguni.

Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hakutakuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu leo. Wakati ibada itakapokwisha, Bwana Mungu na aokoe kila nafsi iliyopotea, na kuponya kila mwili mgonjwa, na kuujaza moyo wa watoto Wake kwa furaha. Hiyo ndiyo sababu tuna imani, Bwana, kuomba katika Jina la Yesu, kwa Mungu Baba yetu, kwa sababu Yeye aliahidi atasikia. Na hii ni kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

13 Katika Injili ya Yohana Mtakatifu, mlango wa 17, na kuanzia kifungu cha 20, ninataka kusoma kwa—kwa kifungu. Nafikiri hiyo ni kweli.

> *Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao.*
>
> *Hiyo …*

Naamini nimefungua mahali pengine. Sasa, samahani kwa muda kidogo tu. Ninatafuta maombi ya Yesu ambayo … Ama, si maombi ya Yesu, hasa, bali kwa ajili ya … Huenda nikaandika hapa kwenye somo langu kitu fulani kibaya. Ni mahali ambapo Yesu aliomba ambapo … ama alikuwa akisema ya kwamba kama mwanamke aliye katika utungu wa kuzaa kwa ajili ya kuzaliwa kwa mtoto wake, kuzaa, kuzaa.

Hiyo ni katika Luka ama Yohana? Jack, ni ipi iliyo ndani yake? [Mtu fulani anasema, "Yohana 16." — Mh.] 16 ya Yohana. Nadhani hiyo ilikuwa ndiyo, lakini haikusikika sana kama hiyo. Ya 16 ya Yohana. ["Kifungu cha 21."] Kifungu cha 21. [Mwingine anasema, "Naam."] Hakika, kifungu cha 21. Hakika. Tuko hapa. Yohana, Yohana Mtakatifu 16:21.

> *Ili kwamba wao … wapate kuwa …*

14 La, Ndugu Jack, hilo bado ni kosa. [Mtu fulani anasema, "Jaribu Yohana, kifungu cha 21." Mwingine anasema, "21." Mwingine anasema, "kifungu cha 21 cha 16." Mwingine anasema, "16." — Mh.] Ni ishirini- … 16:21. Nina kifungu cha 16 cha Yohana Mtakatifu, kifungu cha 21. Lakini ni … Nimekosea? [Ndugu fulani anasema, "Mwanamke huzaa, hivyo ndivyo ilivyo."]

Vema, kuna vurugu katika hii, kuchanganyikana katika Biblia hii. Naam, bwana. [Ndugu fulani anasema, "Wao—wao wamechapisha vibaya." — Mh.] Waliichapisha vibaya. Naam, bwana. [Kusanyiko linacheka.] Unajua nini? Hiyo ni kweli kabisa. Hii hapa Biblia mpya kabisa. Nimeipata tu karibuni. Na ina—ina ninii … Imechapishwa vibaya. [Kurasa 1138-1139 za Biblia ya Scofield ya Ndugu Branham zilikuwa zimeshikamana. Sikiliza *Leo Maandiko Haya Yametimia* 65-0219.]

[Askofu mkuu wa Katoliki akisimama jukwaani, Kasisi John S. [Askofu mkuu wa Katoliki akiwa amesimama jukwaani, Kasisi John S. Stanley, anasonga mbele na kumpa Ndugu Branham Biblia yake, na kusema, "Tu—tulia tu. Kuna sababu ya jambo hilo kufanywa, nanyi mnajua jambo hilo. Mungu atakuonyesha jambo fulani la kuhubiri kutoka kwenye jambo hili, ambalo ni la ajabu sana."—Mh.] Vema. ["Tumia tu yangu hapa, ndugu."] Asanteni. Asanteni, sana. 16:21. Asanteni, sana. Hiyo ni kweli.

> *Mwanamke wakati yeye …*
>
> *Amin, amin, nawaambia, Ninyi mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utafurahi; ninyi mtahuzunishwa, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha.*
>
> Mwanamke azaapo, yu—-yuna huzuni kwa kuwa saa yake imefika; lakini akiisha kuzaa mwana, haikumbuki tena ... ile dhiki—-dhiki, kwa sababu ya furaha ya kuzaliwa mtu ulimwenguni.

Asante, sana, ndugu yangu. Hakika ninathamini jambo hilo. [Ndugu Branham anairudisha Biblia kwa kasisi wa Katoliki — Mh.]

Sasa, huko bila shaka ni kuchapishwa kimakosa hapa katika Biblia; kurasa zimewekwa vibaya. Nami nililipata tu kwenye Biblia yangu ya kale ya Scofield, na nikachukua hili na nikakimbia nalo hapa, dakika chache tu zilizopita, maana mke wangu alinipa tu hii kwa ajili ya zawadi ya Krismasi.

15 Sasa, nataka ku—kuzungumza alasiri ya leo juu ya somo nililotangaza: *Utungu wa Kuzaa*. Sasa, hilo linasikika baya sana, bali liko katika Biblia.

Ninaamini ya kwamba Yesu hapa alikuwa akinena habari zake, kama Yeye alivyosema, "Mtakuwa na huzuni, bali huzuni yenu itageuka kuwa furaha," akizungumza na wanafunzi Wake hapa, akijua ya kwamba kuzaliwa kwa—kwa Ukristo kulikuwa kunakuja. Na sasa mambo ya kale hayana budi kufa, kusudi yaliyo mapya yapate kuzaliwa. Kuwa na cho chote kinachozaa, haina budi kuwa na maumivu ya taabu. Na bila shaka walikuwa watapitia katika uchungu wa dhiki na maumivu makuu, kutoka kwenye torati kuingia katika neema

Kawaida, uzazi wa kawaida ni mfano wa uzazi wa kiroho. Mambo yote ya kawaida ni mfano wa yale ya kiroho. Nasi tunaona, kama tukiangalia hapa nje kwenye—kwenye ardhi, na kuona mti katika nchi, ukikua, ukishindania uzima. Hiyo inaonyesha ya kwamba kuna mti, mahali fulani, ambao haufi, kwa sababu una—unalilia jambo fulani.

Tunaona watu, haidhuru wao ni wakongwe namna gani, ni wagonjwa jinsi gani, wana hali gani, wanalia, wapate kuishi, kwa kuwa inaonyesha kuna uhai mahali fulani ambapo tunaishi—tunaishi milele. Angalia jinsi lilivyo kamilifu.

16 Sasa, katika Yohana wa Kwanza 5:7, ninaamini ndivyo ilivyo, kama sijakosea, ilisema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni: Baba, Neno, na Roho Mtakatifu; hawa watatu ni Mmoja. Kuna watatu washuhudiao duniani, ambao ni maji, Damu, na Roho, nao wanakubaliana katika mmoja." Sasa angalia. Hao watatu wa kwanza *ni* Mmoja. Hao watatu wa pili ni wa duniani, ambao hupatana kwa habari moja. Huwezi kuwa na Baba bila Mwana; huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu. Lakini unaweza kupata maji bila Damu, na Damu bila Roho.

Nafikiri, kote katika nyakati zetu, hii imethibitika kwamba ni kweli; maji, Damu, Roho; kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo hufananishwa au inafanya ninii…au, na kivuli, ambayo hondoa kutoka kwenye kuzaliwa kwa maumbile.

Angalia wakati mwa—mwanamke ama cho chote kile katika utungu wa kuzaa, kwa ajili ya kuzaa. Jambo la kwanza linalotukia, ni kutoka kwa maji, kuzaliwa kwa kawaida; jambo la pili ni damu; halafu uhai unatokea. Maji, damu, roho; na hiyo hufanya kuzaliwa kwa kawaida, kwa maumbile.

17 Na ndivyo ilivyo katika ulimwengu wa kiroho. Ni maji; kuhesabiwa haki kwa imani, kumwamini Mungu, kumpokea kama Mwokozi wako binafsi, na kubatizwa. Pili, ni utakaso wa roho, kwamba Mungu husafisha roho kutoka kwenye vitu vyote vya ulimwengu, na tamaa ya ulimwengu. Na ndipo Roho Mtakatifu anaingia na kutoa Uzao mpya na kukijaza chombo hicho kilichotakaswa.

Kwa mfano, namna hii. Sasa, hilo, niliwaambia. Kile usichoamini, weka kando, kisha ule sambusa. Angalia. Sasa, gi—glasi iko kwenye ua wa kuku. Huichukui tu hiyo na kuiweka mezani mwako na kuijaza na maji ama maziwa. La. Unapoichukua, ni kuhesabiwa haki. Ukiiosha, ni kuitakasa, maana neno la

Kiyunani *kutakasa* ni neno lenye sehemu mbili, ambalo linamaanisha "kuoshwa, na kutengwa kwa ajili ya kutumika." Si *katika* utumishi; *kwa ajili ya huduma*. Halafu unapoijaza, inawekwa katika huduma.

18 Samahani kwa jambo hili sasa, sio kuumiza. Hapo ndipo ninyi Wapilgim Holiness, Wanazarayo mlishindwa kupiga hatua mpaka kuingia kwenye Pentekoste. Mlisafishwa kwa kutakaswa; lakini mlipokuwa tayari kuwekwa katika huduma, kwa karama za kunena katika lugha na vitu vingine, mlizikataa hizo, mkarudi zizini tena. Mnaona? Sasa, hilo—hilo ndilo linalotukia. Daima hufanya hivyo.

Sasa, si kuwalaumu ninyi sasa, lakini ninii—ninataka kutoa jambo hili moyoni mwangu. Na hilo limekuwa likinichoma tangu nilipokuwa hapa, kwa hiyo ni heri nilitoe. Ninii tu, kama neema ya Carl, na Demos na hao wengine, na yenu nyote, ni—nitajaribu kukomboa nafsi yangu kutokana na jambo hilo, unaona, ndipo basi ni juu yenu.

Ya kawaida, yakiwa mfano wa ya kiroho.

Sasa, tunaona basi, na amezaliwa kikamilifu. Wakati mtoto mchanga, kwa kawaida … Sasa wakati maji yanapovuja, haikubidi kumsaidia sana. Na wakati damu inapotoka, haikubidi kumshughulikia sana. Lakini, ili uhai uingie ndani ya mtoto huyo mchanga, huna budi kumpiga kofi la matakoni, na kumfanya apige makelele. Na hiyo ni ninii … Sasa, bila elimu, kwa kuwa ndugu zangu hapa wamefunzwa vizuri sana kwao, kwao, lakini sina budi kuchukua maumbile kuifananisha. Na hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ndilo lililotukia. Inatakiwa kupigwa kofi halisi, kuingiza hili ndani yao.

19 Sasa, hebu chukua kidogo, namna fulani ya mshtuko. Labda, haitakulazimu kumpiga kofi, lakini mshtue tu kidogo. Wazo lenyewe la Yeye kuzaliwa, wakati mwingine, litafanya jambo hilo. Mnyakue, mtikise. Asipoanza kupumua, mpige kofi kidogo, ndipo atapiga mayowe, katika lugha isiyojulikana, kwa nafsi yake, nadhani. Lakini, yeye—yeye, hata hivyo, naye anapiga makelele.

Nami nafikiri kama mtoto akizaliwa tu akiwa—akiwa kimya, hana sauti, hana msisimko, huyo ni mtoto mfu.

Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, mfumo; tuna watoto wengi sana waliokufa. Hiyo ni kweli. Wanahitaji kupigwa kwa Injili, mnaona, na kwa hiyo kuwaamsha, kuwafanya wajirudie, ili kwamba Mungu aweze kuwapulizia pumzi ya Uzima. Na sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli sana. Ni theolojia ghafi, bali ni Kweli, hata hivyo.

20 Kwa hiyo, angalia, katika kuzaliwa kwa mbegu, ile mbegu ya kale haina budi kufa kabla ya ile mpya kuzaliwa. Kwa hiyo, basi, kifo ni jambo gumu, wakati wo wote. Kwa hiyo, ni chungu. Kinauzunisha. Kuzaliwa ni jambo lile lile, kwa sababu unaleta uhai ulimwenguni, na ni—ni kuchungu.

Yesu alisema ya kwamba Neno Lake lilikuwa ni Mbegu ambayo mpanzi alitoka akaenda kupanda. Sasa, sote tunajua jambo hilo. Nami nataka kufundisha hili kama somo la shule ya Jumapili, maana ni Jumapili. Angalia, basi, Neno hili, likiwa ni Mbegu. Lakini, kumbuka, ile—ile mbegu inaleta tu uhai mpya inapokufa.

Na hiyo ndiyo sababu ilikuwa ni vigumu sana kwa hao Mafarisayo kumfahamu Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sababu walikuwa chini ya torati. Na torati ilikuwa ni Neno la Mungu katika umbo la mbegu. Lakini wakati Neno lilipofanyika mwili, na likawa, si torati, bali neema. Sasa, neema na torati haziwezi kuwepo kwa wakati mmoja. Maana, neema iko mbali sana na sheria, sheria hata haionekani. Na kwa hiyo ni vigumu sana kwa Mafarisayo kufa kwa sheria zao, ili kwamba neema ipate kuzaliwa. Lakini haina budi kuondoka. Sheria hizo mbili haziwezi kuwepo kwa wakati mmoja.

Hakuwezi kuweko na sheria inayosema ya kwamba unaweza kutumia selo hii, na nyingine inayosema unaweza kuitumia; moja inasema unaweza, nyingine inasema huwezi. Hizo, haina budi iwe ni sheria moja kwa wakati mmoja. Labda wakati mmoja ungaliweza kuipitia; kwa uangalifu, upite katika hiyo. Lakini wakati huu ni nyekundu. Simama! Mnaona? Na kwa hiyo hakuwezi kuwa na sheria mbili zinazofanya kazi wakati ule ule.

21 Sasa, tunaona ya kwamba daima … Wazo langu sasa kwako, linahitaji uchungu, dhiki, adha. Waangalie hao Mafarisayo waliokufia hiyo torati, kupitia kwenye uchungu, dhiki, adha. Lakini lazima iwe hivyo.

Sasa, tunaona ya kwamba mvua inayoleta matunda juu ya nchi, "Inazaliwa," kama mshairi alivyosema, "katika mashamba ya radi, katika anga zilizochafuka, zenye mawingu mazito hapa na pale." Lakini kama hatungalikuwa na ngurumo na anga zilizochafuka, lile tone dogo la mvua lililotoneshwa ambalo limeinuliwa kutoka baharini na kutoneshwa kutoka kwenye chumvi, halingezaliwa. Inahitaji hiyo radi, milipuko ya ngurumo; kitu hicho cha kutisha kilichochafuka, kinachoparuza, kuzaa lile tone la petali nyororo la maji. Kuzaliwa kunahitaji uchungu. Kunahitaji kufa. Na wakati mawingu yanapokufa, mvua huzaliwa, kwa sababu mvua ni sehemu ya wingu hilo. Moja halina budi kutoweka kusudi lingine lipate kuishi.

Sasa, na ndugu zangu hapa, baadhi yao waliweza, wangeweza kukupa kanuni zote za vitu hivyo. Siwezi.

22 Sasa hebu na tuangalie jambo lingine, kwa thibitisho dogo tu. Nafikiri moja ya maua mazuri sana … Kila mtu ana mawazo yake mwenyewe kuhusu hayo. Lakini nadhani ua maridadi sana ambalo karibu nimepata kuona, ni huko nyuma mashariki, yungiyungi letu la kidimbwini. Ni wangapi wamewahi kuona yungiyungi la kidimbani? Loo, hakuna kitu kama hicho, kwangu mimi. Lakini je! Uliona kile yungiyungi la kidimbwi lilipaswa kuwa? Ninawazia juu ya yale Yesu aliyosema, "Fikirini yungiyungi, jinsi linavyofanya kazi na kusokota, lakini hata hivyo nawaambia, ya kwamba, Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya haya." Kwa kuwa, utukufu wa Sulemani na mavazi yake yote yalikuwa ya kujitengenezea. Lakini yungiyungi, katika uzuri wake, linafanywa zuri na uhai, si vitu fulani vya kujipaka vya kujitengenezea, kujipaka rangi.

Ni kama vile tu wanawake wetu, sidhani inawabidi kuwa na rangi hizi zote za kijani za kujipaka, mwajua, vikonyeza macho, mwajua, nje namna hiyo, na rangi hizo zote za makucha ama—ama sivyo, ninachanganyikiwa na vitu hivyo, vyote usoni mwako, kukufanya mrembo. Urembo ni vile urembo ufanyavyo. Kama utaongeza Matendo 2:4 kidogo, changanya yote pamoja, na Yohana 3:16 kidogo, itashinda kitu cho chote ambacho Max Factor aliwahi kujaribu kurekebisha. Mnaona? Mumeo atakupenda zaidi; kila mtu mwingine atafanya hivyo; nami nina hakika Mungu atafanya hivyo.

23 "Yungiyungi," Yeye alisema, "fikirini, jinsi limeavyo, linavyofanya kazi, halina budi kujisukuma juu." Maskini yungiyungi hili dogo la kidimbwini, angalia mahali linapopitia; uchafu, vinyaa, matope, maji ya matope, maji machafu. Linajipenyeza kupitia hayo yote, chembechembe hii ya uhai, likijipenyeza kutoka kilindi cha kidimbwi ambamo mna vyura na—na ghasia nyingi, na halafu linajipandisha kupitia katika hayo yote. Lakini inapofikia kwenye uwepo wa jua, huzaliwa. Mbegu hiyo ndogo hupasuka ikaingia katika uhai. Haiwezi kufanya hivyo mpaka itakapopitia kwenye utaratibu huo wote. Haina budi kupitia jambo hilo. Hilo ndilo linalolitengeneza, ni kwa sababu jua lenyewe ndilo linalolivuta juu. Na hapo linapofikia juu ya maji machafu kabisa, na vinyaa, na kadhalika, ndipo linafurahi sana. Linatoa tu uhai wake bure. Na ni uhai unaopendeza wakati linapofikia kwenye uwepo wa hilo linalolivuta juu.

Nafikiri huo ni mfano mzuri wa maisha ya Kikristo. Wakati, Kitu fulani kinakutoa ulimwenguni, mpaka siku moja umezaliwa moja kwa moja katika uwepo Wake, na Roho Mtakatifu. Ni jambo zuri iliyoje! Ukijaribu kulisaidia, unaliua.

24 Kama vile kifaranga kidogo cha kuku kinapozaliwa, unajua, kama uliwahi kuona mmoja wa jamaa hao wadogo, nchani kabisa mwa mdomo wake mdogo, ama ndege ye yote anayezaliwa kutoka kwenye yai. Li—linaninii … Linakua, hili ganda la kale la yai. Sehemu za ndani za mayai zilizokomaa sana hazina budi ku—kuoza. Naye hana budi kuchukua maskini mdomo huu mdogo, na kuparuza-paruza mpaka anavunja lile ganda. Tunakuita huko, kujikokota nje, kule chini Kentucky ninakotoka. Kujikokota atoke nje. Kamwe hawajawahi kupata njia bora zaidi. Mnaona? Mnaona? Kwa nini? Ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Ukijaribu kumsaidia, utamwua. Ukilivunja ganda atoke, atakufa. Mnaona? Hana budi kufanya kazi, kujitahidi, na kuvunja atoke.

Hivyo ndivyo Mkristo anavyopaswa kufanya. Si swala la mtu eti kukupa mkono, kukuingiza. Inakubidi ukae pale mpaka ufe, uoze, na uzaliwe katika Ufalme wa Mungu. Ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Huingii kwa kitabu, ama kupeana mikono, na kujiunga, kuhojiwahojiwa, kujilazimisha. Ina—inakubidi tu kuondoka kwenye lile ganda la kale. Angalia, hawajapata njia nzuri zaidi.

25 Hawakupata njia bora zaidi ya mtoto mchanga kupata kile anachotaka mbali na njia ya Mungu kwa ajili yake. Sasa, wakati mtoto huyo mdogo anapozaliwa, ungeweza kuweka kengele chini hapa karibu na kitanda chake kidogo, useme, "Mwanangu mdogo, katika njia hii mimi ni mwa— mwanatheolojia. Nimesoma vitabu juu ya kulea mtoto mchanga. Na, hebu nikwambie, wewe ni mtoto wa kisasa. Umezaliwa katika nyumba ya kisasa, na mzazi wa kisasa. Unapokuwa na njaa, au unapohitaji mama au mimi, piga tu kengele hiyo ndogo." Haitafaa kitu kamwe. Njia pekee ambayo iaaweza kupata kile anachotaka, ni kukililia. Hiyo ndiyo njia ya Mungu.

Na hivyo ndivyo tunavyopata kile tunachotaka, ni kukililia. Lia. Usione haya. Sema, "Nina njaa ya Mungu." Sijali kama mashemasi, wachungaji, ama ye yote yule, piga makelele, hata hivyo. Akina Jones wameketi pale; inaleta tofauti gani? Lia kabisa, hiyo ndiyo njia tu iliyopo ya kukipata, mpaka upate msaada. Yeye alifundisha jambo hilo wakati alipokuwa hapa duniani, mwajua, juu ya yule hakimu dhalimu.

26 Tone dogo la umande, sijui kanuni yake. Labda kungekuwa na sayansi hapa ya … Nitasema tu jinsi ninavyofikiria. Huenda ikawa ni namna fulani ya anga lililochafuka kwa mawingu yaliyosongamana katika usiku wenye giza, nayo yanaanguka chini. Na yakianguka, tone linazaliwa usiku. Lakini asubuhi, liko pale, baridi, na linatatetemeka, kwenye unyasi mmoja mdogo, ama likining'inia kwenye kamba yako ya kuanikia nguo. Lakini hebu acha tu jua liangaze mara moja, je! Uliona jinsi inavyokuwa na furaha? Linametameta tu na kutetemeka. Kwa nini? Lnajua ya kwamba ni kwamba nuru ya jua italirudisha nyuma mahali lilipokuwa hapo mwanzo.

Na ndivyo ilivyo kwa kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu. Kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo, wakati Nuru inapoenea juu yetu, kwamba tunafurahi, kwa sababu tunajua tunarudi tunakotoka, kutoka kifuani mwa Mungu.

Linaweza kumetameta kwa furaha, wakati jua linapolipiga, bila shaka, tukijua linaelekea linakotoka.

Mambo madogo madogo yasiyofaa, bali tungeweza kuendelea nayo, lakini hebu tupate kitu kingine.

27 Tunajua ile mbegu ya kale ni, haina budi, kabla ile mbegu mpya haijaweza kutoka kwenye ile mbegu ya kale, haina budi kuoza, kabisa. Si kufa, bali tu kuoza baada ya kufa. Tunajua jambo hilo kuwa ni kweli.

Hilo ni jambo lile lile katika Kuzaliwa upya. Haturudi nyuma kamwe, bali tunasonga mbele unapozaliwa mara ya pili. Na hiyo ndiyo sababu ninafikiri, leo, tunaninii (wengi sana) si wengi sana, hasa, Wanazaliwa upya halisi, ni kwa sababu ile mbegu, labda, italihurumia Neno ama mtu, lakini wao hawataki kuoza kutoka kwenye ule utaratibu wa zamani ambamo waliokuwamo. Hawataki kutoka kwake. Wanataka kukaa katika mfumo wa kale, na kudai Kuzaliwa upya, ama Ujumbe wa wakati huu. Tuliona jambo hilo chini ya Luther, Wesley, Wapentekoste, na nyakati zingine zote. Wao wangali wanajaribu kushikilia ule mfumo wa kale, na kudai Hili. Lakini ule wakati wa mfumo wa kale hauna budi kufa, kuoza, kusudi uzae ule mpya. Wangali wanataka kushikilia.

28 Angalia. Wanajua mfumo wa kale umekufa, bali hawataki kabisa kuoza watoke humo. Sasa, kuoza, ni wakati ambapo kweli imeondolewa. Wakati ninii … *Madai* yanatolewa, ya kwamba wamezaliwa upya, bali dai ni ishara tu ya kuzaliwa. *Kuoza*, kunaleta Kuzaliwa upya. Hatuna budi kuoza kutoka kwake, kama tu tulivyofanya katika nyakati zote, kupitia kwa Wesley, na kadhalika.

Lakini, jambo ni kwamba, baada ya hapo, Kuzaliwa upya kunazaliwa. Wesley ama … Luther alikuja na neno moja, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Vema, asingeweza tena kushikilia kwenye ule mfumo wa kale. Ilibidi atoke kwake.

Na ndipo wakati Wakalvini walipoliingiza kanisa la Kianglikana katika hali kama hiyo, chini ya fundisho la Kikalvini, mpaka Mungu akainua fundisho la Kiarmenia, ambalo lilikuwa ni John Wesley. Mfumo wa kale ulipaswa kufa, kusudi ule mpya upate kutokea.

Na wakati wa Wesley ulipoisha, na nyakati zote ndogo, ama majani yaliyochipuka kwenye ubua, ama kishada, katika wakati wa Wesley. Mnaona, wakati Pentekoste ilipotoka pamoja na kurudishwa kwa karama, iliwabidi watoke kwenye Baptisti, Presbiteri, Pilgrim Holiness, Wanazarayo, kanisa la Kristo, linavyojiita, na hayo yote. Iliwabidi watoke katika hayo, waoze kabisa, kusudi wakubali Kuzaliwa upya.

29 Daima unaitwa mwenda wazimu. Lakini ni kama vile Paulo alivyosema wakati alipooza kutokana na kile alichodai wakati mmoja. Kasema, "Kwa njia ambayo inaitwa uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Katika njia ile ambayo waiita uzushi! Mnaona? Alikuwa amekubali Uzima mpya, kwamba Agano la Kale lilikuwa limezaa lile Jipya, naye ilimbidi kuoza kutoka kwa la Kale na kulifanya tu kivuli. Kusudi kuwa …

Hapo ndipo tu tulipo sasa. Sasa, nivumilieni. Lakini hilo ndilo wazo langu. Makanisa yamekuwa ya kimifumo sana hata huwezi kuingia kwenye moja isipokuwa wewe ni mshiriki wake. Huna budi kuwa na kadi ya ushirika, ama namna fulani ya utambulisho. Na kwa kuamini jambo hili, mlango pekee ambao karibu nimeufungua ni hawa Wafanyabiashara. Na mradi tu wao si madhehebu, ninaweza kuingia pamoja nao, lakini, na kupata kuuleta Ujumbe, ambao ninajisikia uko moyoni mwangu, kwa watu. Lakini limekuwa la utaratibu sana. Nami nawapenda ninyi Wapentekoste. Na pentekoste si dhehebu, hata hivyo. Unajiita tu hivyo. Pentekoste ni tukio na si dhehebu.

Lakini, mnaona, jambo ni kwamba, ni vigumu sana kwa watu wengi. Wakati wanapoliangalia na kuliamini, na kuliona limeonyeshwa dhahiri sana na Mungu, katika Neno, hata hivyo, ni vigumu sana kuoza kabisa na kutoka katika kitu hicho ulichokuwa ndani yake. "Ningefanya nini? Nitapata wapi chakula changu?"

Nini? Mungu ndiye chakula chako. Mungu ndiye kitu cha kushikilia. "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake." Nitaliachia hapo. Mnajua yale ninayonena.

30 Tunaambiwa na manabii wa Mungu kwamba tunapaswa kuwa na nchi mpya, Mbingu mpya na nchi mpya. Kama unataka Maandiko juu ya jambo hilo, ni Ufunuo 21. Ningeweza kunukuu kwa ajili yenu, ninalo hapa. Yohana alisema, "Niliona Mbingu mpya na nchi mpya: kwa kuwa mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zilikuwa zimepita." Ilikuwa imeondoka. Sasa, kama tutakuwa na nchi mpya, nchi ya zamani na nchi mpya haviwezi kudumu kwa wakati ule ule. Ama, ulimwengu mpya na ulimwengu wa zamani hauwezi kuwepo kwa wakati mmoja. Hakuwezi kuwa na taratibu mbili za ulimwengu pamoja kwa wakati mmoja. Sasa, kusudi upate ile nchi mpya, ile ya kale haina budi kufa. Sasa, kama ile ya kale haina budi kufa, basi inapata utungu wa kuzaa kwa ajili ya ile mpya sasa.

31 Halafu basi kama daktari alienda kumchunguza mgonjwa aliyekuwa katika uchungu wa kuzaa sasa, ninii … moja ya mambo ambayo daktari angefanya. Ambapo, ninazungumza mbele ya wawili ama watatu, niwajuao, madaktari wazuri wa madawa hapa, madaktari Wakristo. Nami ni—ni—ningewauliza jambo hili. Moja ya mambo ambayo daktari hufanya, baada ya kuwa amempima mgonjwa, ni kupima muda wa utungu, utungu wa kuzaa. Yeye hupima muda wa utungu, jinsi mmoja unavyokaribia mwingine, jinsi kila mmoja unavyokuwa mchungu zaidi. Mmoja ni mkali zaidi kuvumilia kuliko huo mwingine. Unaofuata, mkali zaidi, unakaribia karibu zaidi na mwingine. Hivyo ndivyo anavyopima hali hiyo, kwa utungu wa kuzaa.

Vema, kama ulimwengu hauna budi kuachilia ulimwengu mpya uzaliwe, hebu tuchunguze tu baadhi ya utungu wa kuzaa tulio nao duniani, na ndipo tutaona kuhusu ni siku gani na una umbali gani katika utungu wake.

32 Vita vya Kwanza vya Dunia vilionyesha utungu mkubwa wa kuzaa. Ilionyesha moja ya utungu wa kwanza wa kuzaa kwake ukipata utungu wa kuzaa. Kwa sababu ya wakati huo kwake, tulikuwa tumeleta mabomu, na tulikuwa na bunduki, na gesi ya sumu. Nanyi mnakumbuka. Labda wengi wenu hamwezi. Nilikuwa mvulana mdogo tu mwenye umri wa kama miaka minane, lakini ninakumbuka wakinena juu ya hizi za haradali na klorini, na kadhalika. "Jinsi ilivyoonekana tu kama ingeanza tu na," wakasema, "ingeiteketeza dunia nzima. Ingeua kila mtu. Vema, huenda ikawa ni ku—ku—kuachiliwa kwa hiyo, upepo tu ukiivumisha kote duniani." Na jinsi kila mtu alivyoogopa kufa kwa hiyo silaha kuu ya gesi ya sumu! Dunia ilipitia, ikawa na utungu wake wa kwanza wa kuzaa.

Nasi tunaona sasa, tumekuwa na vita vya pili, Vita vya Ulimwengu, na maumivu yake yalikuwa makubwa zaidi. Unakuwa wa kutisha zaidi wakati wote, utungu wa kuzaa wa dunia. Dunia ilikuwa karibu iachilie, wakati wa bomu la atomiki, kwa maana lingeangamiza mji mzima. Utungu ulikuwa ni mkubwa zaidi kuliko utungu wa Vita vya Kwanza vya Dunia, katika kuiharibu nchi.

33 Sasa, inajua ya kwamba wakati wake wa ukombozi umekaribia. Hiyo ndiyo sababu ina wasiwasi sana, imechanganyikiwa, kama ilivyo, ni kwa sababu kuna bomu la haidrojeni, na makombora ya angani ambayo yangeweza kuuangamiza ulimwengu mzima. Taifa moja linaogopa lingine, haidhuru ni dogo jinsi gani. Wana makombora hayo wanayodai yataninii tu … Moja ya hayo. Wanaweza kuyaongoza kwa nyota na kuyaangusha mahali po pote ulimwenguni wanapotaka.

Urusi, kama nilivyosikia kwenye taarifa ya habari, hivi majuzi, inadai ya kwamba inaweza kuliangamiza taifa hili, na—na kuzuia hizo atomi ama vitu hivyo kuangamiza taifa lake. Hatujui la kufanya kuhusu jambo hilo. Kila mtu anatoa madai haya, na ndivyo ilivyo.

Sayansi ya watu imeingia katika maabara kuu ya Mungu, mpaka watajiangamiza wenyewe. Mungu huachilia, daima huacha hekima ijiangamize. Mungu haangamizi chochote. Mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa hekima, kama alivyofanya hapo mwanzo, akichukua hekima ya Shetani badala ya Neno la Mungu.

Sasa, dunia inajua haina budi kuachilia iangamie. Haiwezi kustahimili jambo hilo.

34 Urusi, ninaamini, ingeliangamiza taifa hili leo, kama ilidhani ya kwamba ingeweza kuliangamiza, na kisha kujihifadhi. Yoyote ya hayo mataifa madogo yangeweza kufanya jambo hilo. Lakini, wanaogopa, kwa sababu wanajua ya kwamba ulimwengu huu hauwezi kusimama katika mzunguko wake chini ya hali kama hizo.

Kwa hiyo, ulimwengu unajua ya kwamba utungu wake wa kuzaa ni mkubwa sana, hauna budi kuachilia. Kutakuwa na kuzaliwa kupya, kuzaliwa, karibuni. Ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nimechoshwa na huyu. Ye yote … mtu yeyote anajua ya kwamba—hapa ndipo mahali pa mauti na huzuni, na kila namna ya hitilafu, na kadhalika. Nina furaha kwamba haina budi kuachilia. Nina furaha kwamba wakati umewadia. Kama Yohana, wa kale, alivyosema, "Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu."

35 Sasa, haina budi kuoza, bila shaka, kama nilivyosema, kusudi ilete uzao mpya. Angalia vile ilivyooza. Angalia, ndugu zangu! Imeoza kabisa. Siasa zake na taratibu zake zimeoza ziwezavyo kuwa. Hakuna mfupa mzima ndani yake, katika mifumo yake ya ulimwengu, siasa zake na siasa zake za kidini, na chochote kile. Mmoja anasema, "Mimi ni wa Democrat. Mimi ni wa Republican. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbatisti." Mbona, kitu hicho chote kimeoza kabisa. Hapana budi kuwe na kitu fulani kitakachotolewa. Haiwezi kusimama. Kama ukiweka George Washington ama Abraham Lincoln katika kila jimbo katika Marekani hii, bado isingeweza kurudi. Haikomboleki.

Kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuisaidia, hicho ni Kuja kwa Muumba. Amina.

Inajua haina budi kuachilia. Iko katika uchungu na dhiki. Mtu hajui la kufanya. Mmoja anaangalia *huku*, na mwingine *kule*, na kila kitu. Mmoja anamwogopa mwingine. Mtu akijaribu kufanya jambo fulani kumwangamiza *huyu* mwingine. *Huyu* akijaribu kupingana na *huyo*, kuangamize mwingine. Mpaka, sasa wameiweka mikononi mwa watu wenye dhambi, ambao wangeweza kuiangamiza dunia nzima katika muda wa dakika tano. Mnaona? Kwa hiyo inajua haiwezi kustahimili jambo hilo. Watu wanajua haiwezi

kustahimili jambo hilo. Na ulimwengu unajua ya kwamba watafanya, watafanya hivyo.

36 Kwa kuwa, Mungu alisema ilikuwa hivyo. "Mbingu zote na nchi zitateketezwa kwa moto." Itakuwa ni kukarabatiwa kwa kitu hicho chote, kusudi ulimwengu mpya uzaliwe. Mungu ametabiri jambo hilo.

Imeoza, katika mifumo yake yote, nayo haina budi kufanya hivyo, ipate kuoza.

Hiyo ndiyo sababu hiyo, nilisema, ina wasiwasi sana na imeiva usoni, na inafadhaika. Na matetemeko ya nchi, kila mahali, na huku na huko pwani. Na mawimbi makubwa huko Alaska, na kutetemeka huku na huko katika pwani, kwa matetemeko ya ardhi na kadhalika. Na watu wakiandika, "Je! tuhame? Je! tuhame?" Mnaona? Hawajui la kufanya. Hakuna mahali pa salama ila Pamoja, hapo ni katika Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Na kuna jambo moja tu ambalo ni mahali pa salama, na hilo ni Yeye. Wote walio nje ya Hapo wataangamia, kwa hakika tu kama Mungu alivyosema.

37 Sasa hebu na tuangalie kwenye Kitabu cha Daktari, kama iko katika hali ya namna hii, na tuone kama jambo hili linapaswa kutukia wakati nchi mpya itakapozaliwa. Mathayo 24, katika Kitabu cha Daktari, ambacho ni Biblia, na hebu tuone kile kilichotabiriwa, dalili zake zingekuwaje.

Sasa, kama daktari anajua dalili za kuzaliwa kwa mtoto … Na yapata wakati ambapo mtoto atakuja, yeye huandaa kila kitu, kwa sababu anajua ya kwamba huo ndio ule—ule wakati mtoto atakapozaliwa. Kwa sababu, dalili zote zinaonyesha; ma—maji yametoka, damu. Na sasa ninii … Ni wakati. Mtoto ameshuka, na ni wakati wa mtoto kuzaliwa. Na kwa hiyo yeye huandaa kila kitu kwa ajili yake.

Sasa, Yesu alitwambia hasa yale hasa yangetukia wakati huu. Sasa, Yesu alitwambia vile hasa ingetukia kwenye wakati huu. Alitwambia, katika Mathayo 24, ya kwamba Kanisa, Kanisa la kweli, na kanisa hilo lingine, lingekuwa…na Kanisa la kawaida, Kanisa la kiroho, "Wangefanana sana, hao waigaji, mpaka ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini." Kama ambavyo ilikuwa katika siku za Nuhu, "walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa," na uasherati huu wote wa ulimwengu tunaouona siku hizi. Biblia, kile Kitabu, Kitabu cha Daktari kilisema ingetukia. Kwa hiyo, tunapoona jambo hili likitukia, tunajua ya kwamba kuzaliwa kumekaribia. Haina budi kuwa. Naam, bwana. Sasa, tunaangalia jambo hilo, kama—kama taifa; si kama taifa, bali ulimwengu.

38 Sasa, Israeli, kanisa, hebu tuanze nayo kwa dakika chache. Na hebu tuifuatilie kwa dakika kumi zifuatazo, labda. Israeli ilikuwa na utungu wa kuzaa chini ya kila nabii aliyekuja duniani. Ilikuwa na utungu wa kuzaa kwa Ujumbe wake. Kwa maana ilifanya nini? Nabii alikuwa na Neno. Nayo—nayo ilikuwa imepanda upuuzi mwingi sana na kuunda mashirika mengi sana ya kwake, mpaka nabii huyu akaitikisa hata kwenye msingi wake. Walichukiwa na kila mtu. Kwa hiyo, basi, wakati Mungu alipomtuma nabii, kanisa lenyewe liliingia katika utungu wa kuzaa. Kwa sababu, nabii, "Neno la Bwana humjia nabii, na yeye peke yake." Hiyo ni kusema, Neno lililonenwa kwa ajili ya siku hiyo linadhihirishwa na nabii wa wakati huo, daima limedhihirishwa. Na, makanisa, yanajenga mifumo mingi sana kuzunguka Neno, hata akaitikisa ikatoka kwenye msingi wake wakati alipokuja. Ilikuwa na utungu wa kuzaa.

Ilikuwa ni kitu gani? Rudini kwenye Neno! Rudini kwenye Uzima! Mifumo haina Uzima. Ni Neno la Mungu tu lililo na Uzima. Taratibu zilizojengwa kulizunguka, ambapo hapana Uzima. Neno ndilo linalohuisha. Ujumbe Wake ulitikisa mabaki kurudi kwenye Neno. Kundi dogo litatokea na kuamini. Wakati mwingine, labda … Katika wakati wa Nuhu, yapata watu wanane tu. Lakini, hata hivyo, Mungu aliwatikisa waliosalia. Na, kuangamiza, hao wengine iliwabidi kutikiswa sana.

39 Ilifanya hivyo, kote katika nyakati, mpaka hatimaye kanisa likawazalia Mtoto Mwanamume, na Mtoto huyo Mwanamume alikuwa Neno, Lenyewe, lililofanyika mwili. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Alimshinda kila pepo, kila nguvu juu ya nchi, iliyomjia, akiwa na Neno la Baba pekee. Kila jaribio ambalo Shetani alimpa, alimkemea Shetani; si kwa nguvu Zake—Zake Mwenyewe alizokuwa nazo, bali kwa Neno la Mungu. "Imeandikwa … Imeandikwa … Imeandikwa …" Kwa kuwa Yeye alikuwa Neno.

Wakati Shetani alipomrukia Hawa, yeye hakuwa Neno, kwa hiyo alishindwa. Wakati aliporuka dhidi ya Musa, ilifanya jambo lile lile. Lakini wakati alipomgonga Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa na volti elfu kumi. Ziling'oa manyoya yaliyolegea, wakati aliporudi na kusema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, lakini kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'" Huyo hapo Mtoto Mwanamume, aliyefanyika mwili. Neno la Mungu la Milele, Mwenyewe, aliyedhihirishwa katika mwili wa nyama hapa duniani, kuwakilisha Neno.

40 Hivyo ndivyo Yeye alivyojua yale yaliyokuwa mioyoni mwao. Hivyo ndivyo alivyoweza kumwambia Filipo mahali alipokuwa, yeye alikuwa ni nani. Angeweza kumwambia Simoni Petro alikuwa ni nani. Akamwambia yule mwanamke kisimani. Kwa nini? Yeye alikuwa Neno. Sawa. Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 4, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, linachoma na kuyagawanya mafuta ya mifupa, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

Mbona, hao makuhani Mafarisayo waliopofushwa hawakuweza kuona ya kwamba Huyo alikuwa ni

Neno lililodhihirishwa, kwa maana walikuwa wamejifungia katika ukuhani na mfumo. Na utaratibu wa kale ulipaswa kuachilia. Ilikuwa ni Neno, bali kile kilichoahidiwa kilikuwa kimetimizwa. Kwa hiyo kama kimetimizwa, hakina budi kuoza. Ni ganda. Ile Mbegu iliendelea.

Musa asingeweza kuuleta ujumbe wa Nuhu. Wala Yesu asingeweza kuuleta ujumbe wa Nuhu, kwa sababu ulikuwa ni wakati mwingine. Na ile mbegu ya kale ilikuwa sahihi, bali ilitimiza kusudi lake na ilikuwa imekufa na imekwisha. Kule kugeuzwa kutoka la kale kuingia kwenye lile jipya, ambapo Uzima ulikuwemo, ndilo jambo lililokuwa likiwatia watu wasiwasi, ndilo bado linalowasumbua siku hizi.

Sisi hatujengi ukuta, kama vile tunavyoanza na ujumbe wa Luther, twende moja kwa moja kwenye mstari mnyoofu, ama ujumbe wa Kipentekoste. Sawa. Tunapiga kona. Tunajenga jengo. Neno la Mungu ndilo ramani. Kila mtu anaweza kujenga mstari ulionyooka, lakini inahitaji mwashi kupiga kona. Inahitaji nguvu za Mungu kufanya hivyo. Inahitaji mpakwa mafuta kutoka Mbinguni, apate kushushwa kufanya jambo hilo. Imekuwa hivyo, katika kila wakati. Na katika wakati wa manabii, Neno la Mungu huja kupitia kwa hao manabii, nao wanapiga kona hizo, wakafanya tofauti hizo. Lakini wajenzi walitaka kujenga ukuta. Si ukuta, hata kidogo. Ni jengo, jengo la Mungu.

41 Sasa, tunajisikia na tunajua ya kwamba Hii ni Kweli, ya kwamba mifumo ilikuwa imeoza katika kila wakati. Na kila moja wa mifumo yao ilibidi ioze na kufa, mpaka ilipolizaa Kanisa hilo. Kutoka kwenye mchafuko huo uliooza kulitokea Neno, Lenyewe. "Neno la Bwana liliwajia manabii." Kamwe halikuwajia kwa makuhani; Liliwajia manabii.

Na angalia, na wakati lilipofanya hivyo, hatimaye Neno hilo lilizaliwa hapa katika mwili wa kibinadamu. Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Yeye alikuwa Neno. Manabii ni sehemu ya Neno, Neno la wakati wao. Sisi, leo, sisi ni sehemu ya Neno, ambao tunalifuata Neno. Lakini Yeye alikuwa utimilifu wote wa Neno. Yeye alikuwa Neno. Yeye alisema …

Wakati walipokuwa wakimshtaki, akijifanya sawa na Mungu, maana Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, walimwambia, "Vema, unajifanya Mwenyewe Mungu."

Yeye alisema, "Je! Haikuandikwa katika torati zenu, ya kwamba mnawaita hao ambao Neno la Mungu liliwajia, 'miungu,' manabii? Nao walikuwa hivyo. Basi mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?"

42 Ambapo, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa katika Mwana wa Mungu. Yeye alikuwa dhihirisho kamili la Mungu. Hivyo ndivyo hatimaye … Utungu wa kuzaa chini ya hao manabii, mbona, wao wakiwa ni Neno, walielekeza kwenye utimilifu wao wenyewe, utimilifu wa Neno. Na kisha hatimaye taratibu hizo zikafa, mpaka, "Neno likafanyika mwili likakaa kwetu."

43 Angalia vile lilivyoonyeshwa katika Yakobo. Angalia vile lilivyoonyeshwa katika Yusufu, hasa. Alipendwa na ndug-…baba yake; akachukiwa na ndugu yake, bila sababu. Yeye alikuwa wa kiroho, angeweza kutabiri mambo, na kufasiri ndoto. Asingeweza kujizuia kuwa hivyo. Yeye alizaliwa tu hivyo. Alichaguliwa tangu zamani kuwa hivyo. Lakini, alichukiwa na ndugu zake, na hatimaye akamwuuza kwa vipande thelathini vya fedha, karibu vipande thelathini. Naye akainuliwa, akaketi mkono wa kuume wa Farao. Aliangalia gerezani mwake, kulikuwako na mnyweshaji na mwokaji; mmoja alipotea na mmoja akaokolewa.

Yesu katika gereza Lake, msalabani; mmoja alipotea, mmoja aliokolewa. Kweli kabisa. Kisha akainuliwa mpaka mbinguni na kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Na wakati atakapoondoka tena, kutakuwa na sauti itakayotoka, "Pigeni magoti," na kila ulimi ukiri.

Na wakati Yusufu alipoondoka kwenye kiti cha enzi na kuanza kwenda mbele, parapanda ililia, na kila goti ilibidi lipigwe. "Yusufu alikuwa akija."

44 Kwa hiyo, siku moja ile Baragumu kuu ya Mungu italia, waliokufa katika Kristo watafufuka, na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri kwa Neno hili. Lakini Yeye anakuja kwa ajili gani? Anakuja hapa kwa sababu gani?

Angalia, yeye alileta Neno hili kamili ambalo lilifanyika mwili, chini ya utungu wa kuzaa wa manabii ambao walipiga makelele, "Yeye yuaja! Yeye yuaja! Yeye yuaja!"

Sasa, lakini ilikuwa bila nabii kwa miaka mia nne, kulingana na historia na Maandiko, kutoka Malaki hadi Yohana. Walikuwa tu na wanatheolojia, makuhani, wachungaji. Sasa hapa tunaweza kuwazia, bila jambo hilo, utaratibu wake ulikuwa umeoza jinsi gani, miaka mia nne bila Ujumbe wa moja kwa moja, wa BWANA ASEMA HIVI, kutoka kwa Mungu. Kwa hiyo, makuhani, manabii, na kadhalika, walikuwa wameika katika hali mbaya sana. Ilikuwa imeoza.

45 Ndipo Yohana, yule Eliya aliyeahidiwa wa Malaki 3, si Malaki 4. Malaki 3, maana Yesu alisema jambo lile lile katika—katika Mathayo sura ya 11.

Wakati jicho la Yohana la tai lilipotiwa utando, kama ninavyoamini kitabu cha Pember kiitwacho *Nyakati za Mwanzoni* kinavyosema. Naye akasema, "Nendeni mkamwulize kama Yeye Ndiye, ama tumtazamie mwingine." Mnaona?

Naye akasema, Yesu, baada ya kuwarudisha wanafunzi wake, baada ya kuwaambia wakae mkutanoni na kuona kilichotukia. "Nanyi nendeni, mwelezeni Yohana mambo haya. Na heri yeye asiyechukizwa."

Aligeuka akawaangalia wanafunzi Wake na watu aliokuwa akiwazungumzia. Yeye alisema, "Mlitoka kwenda kuona nini wakati mlipoenda kumwona Yohana?" Akasema, "Je, mlitoka kwenda kumwona mtu mwenye mavazi mwororo?" Naye akasema, "Ninawaambia, hao ni wale wanaokaa katika majumba ya wafalme." Yeye alisema, "Je, mlitoka kwenda kuona m—m—mwanzi uliotikiswa na upepo?"

Kwa maneno mengine, kila kitu kidogo kilichozuka, kilimtikisa? "Nitakwambia, kama utakuja tu na kujiunga na kundi letu, tunaweza kukupa mshahara bora zaidi." Si Yohana. "Kama hutahubiri dhidi ya *hili* na *lile*, vema, unaweza kujiunga na makundi yetu." Si Yohana.

Kasema, "Basi mlitoka kwenda kuona nini, nabii? Nami nawaambia, zaidi ya nabii. Kwa kuwa kama mnaweza kulipokea, huyo ndiye aliyenenwa habari zake na nabii, akisema, 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia.'" Hiyo ni Malaki 3:1.

Si Malaki 4, hata kidogo. Hiyo ni tofauti. Maana, huyo Eliya akija, ulimwengu utateketezwa mara moja, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu.

46 Sasa, angalia. Ujumbe wake haukuwatikisa sana kutokana na usingizi wao wa kidini. Walisema tu, "Kuna mtu mwenda wazimu kule chini. Tulimpitia, hivi karibuni. Alijiita kichaa; yeye anajaribu kuwazamisha watu kule chini majini. Mnaona? Mbona hakuna kitu kwa mzee huyo. Mbona, hata hana nguo nzuri. Yeye amejizungushia ngozi ya kondoo. Vema, yeye ni maskini kama vile bata mzinga wa Ayubu. Mbona, ni seminari gani aliyopata kutoka? Kadi gani ya ushirika? Hata hatutashiriki katika mikutano yake. Tutamwacha tu asimame huko chini, afe kwa njaa." Mnaona? Ulimwengu haujabadilika sana, wala mifumo. A-ha. "Lakini tutamwacha tu akae kule chini. Yeye hana ninii …"

Unajua ni kwa nini hakujua? Kumbuka, baba yake alikuwa ni kuhani. Lakini kwa nini hakufuata utaratibu wa baba yake, ambao ulikuwa ni desturi kwa watoto kufanya katika siku hizo? Kwa sababu alikuwa na kitu fulani, Ujumbe mkubwa mno. Alikuwa amtambulishe Masihi, kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuwa amesema hivyo. Hao wachache waliosalia waliokuwa wamerudishwa na Ujumbe wa Gabrieli, sehemu zile, walijua ya kwamba hilo lingekuwa namna hiyo. Kwa hiyo tunaambiwa, akiwa na umri wa karibu miaka tisa, alienda jangwani. Baada ya kumpoteza baba yake na mama yake, kwamba alienda jangwani, maana ilimbidi kusikia hasa.

Maana, katika lile jengo kubwa mno la kitheolojia pale, wangalisema, "Sasa, ninajua ya kwamba wewe unapaswa kuwa ndiye utakayemtangaza Masihi. Isaya alisema ulikuwa unakuja, kwa hiyo utakuwa sauti hiyo. Sasa, hivi hudhani ya kwamba Ndugu Jones hapa anatimiza hilo hasa?" Naye angeshawishika kwa urahisi.

Lakini yeye hakujifunza kamwe yoyote ya mifumo yao. Ujumbe Wake ulikuwa muhimu sana. Alitoka akaenda nyikani, kukaa.

47 Angalia. Ujumbe Wake haukuwa kama wa mwanatheolojia. Yeye alitumia mifano. Yeye alisema, "Loo, enyi kizazi cha nyoka." Akiwaita hao makasisi, "nyoka." Hiki, kimojawapo cha mambo mabaya aliyoona nyikani, kimojawapo cha vitu vilivyo na hila, vinavyonyemelea, kilikuwa ni nyoka. Naye akawaza, "Huo ndio hasa mfano mzuri sana wa kulinganisha ninaojua." Yeye alisema, "Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi na hasira itakayokuja? Msianze kusema, 'Sisi ni mali ya hiki na kile,' kwa maana Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." "Mawe haya," yale aliyopata nyikani na ufukoni mwa kijito kidogo.

"Pia shoka," kitu alichotumia nyikani, "limewekwa kwenye shina la mti," kitu alichoona nyikani. "Kila mti usiozaa matunda mema," anajua mahali alikopata kuni zake, unaona, "hukatwa na kutupwa motoni," alitoa kuni kwake. Mnaona? Ujumbe Wake haukuwa wa kasisi, hata kidogo. Ulitokana na maumbile huko, nyikani.

Lakini alikuwa na Ujumbe wa kutangaza, naye alikuwa na imani katika Ujumbe wake, kusema, "Yule Masihi, apaswaye kuja, na, hata, Yeye yupo papa hapa miongoni mwenu sasa. Ninawaambia, yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu, ambaye hamumjui, ambaye sistahili kuchukua viatu Vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

"Yeye ni nani, Yohana?"

"Sijui."

48 Lakini siku moja, akaja kijana mwanamume akishuka kwenda mtoni, Mtu aliyeonekana wa kawaida.

Katika tu … Mzee Yohana Mbatizaji alikuwa amesimama pale, yule nabii mzee aliyebarikiwa, naye akatazama ng'ambo ya Yordani. Yeye alisema, "Tazama, huyo hapo Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

"Unamjuaje, Yohana?"

"Yeye huko nyikani, aliyeniambia niende nikabatize majini, alisema, 'Yeye utakayemwona akishukiwa na Roho, Huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.'"

Ujumbe wake haungetokana na msimamo wa kitheolojia wala utaratibu uliotungwa na binadamu. Ilibidi uje moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

Kwa kuwa, Ujumbe wake haukuwatikisa sana. Wao walifikiria, "Loo, yeye alisema aliona hilo. Ninatilia shaka sana. Sikuona kitu. Nikaangalia. Loo, jamani! Nisingeweza kuona cho chote kuhusu jambo hilo," makuhani na hao wengine wakasema.

Lakini Yeye alimwona, na tunajua sasa ya kwamba yeye alimwona. Hakika, alifanya hivyo. Lakini unaona ulimpata nani?

Haukuwatikisa hata kidogo watoke katika usingizi wao. Waliendelea moja kwa moja, wakamkata kichwa, vivyo hivyo. Lakini hau—haukuwashtua kamwe.

49 Lakini ulipata wale masalio, wale ambao walikuwa na Uzima ndani yao, lile kundi dogo, Ana na—na Simeoni, na wachache wa hao waliokuwa wakikungoja Kuja kwa Bwana. Naye Ana, hekaluni, kipofu, nabii mke aliyemtumikia Bwana kwa maombi. Na halafu siku moja wakati alipokuwa katika Roho …

Na Simeoni alikuwa ametabiri na kusema, mwanamume mzee, alisema, "Roho Mtakatifu aliniambia ya kwamba sitaona mauti hata nitakapomwona Kristo wa Bwana."

Mbona, baadhi ya makuhani, mnajua, walisema, "Maskini mzee yule, yeye kidogo amerukwa na akili, mnajua. Mbona, yeye ameweka mguu mmoja kaburini sasa, na huo mwingine unateleza. Mbona, mwacheni tu. Yeye amekuwa mzee mwenye heshima. Lakini kwa namna fulani yeye ni …"

Lakini, unaona, alikuwa na kitu gani? Ilifunuliwa kwake na Roho Mtakatifu.

Hilo ndilo jambo lile lile ambalo limefunuliwa kwenu ninyi watu alasiri ya leo. Roho Mtakatifu alikuleta hapa kwa sababu fulani. Wale … Roho Mtakatifu! Waangalie hawa makuhani na makasisi hapa kutoka Methodisti, Baptisti, Katoliki, na wote. Waliongozwa na Roho Mtakatifu. Wakati umewadia. Kwa hiyo Roho Mtakatifu akawatokea, nao wamekuwa wakimtazamia, wakiona njaa. Halafu, katika ninii tu …

50 Siku moja, unajua, hakuwa na televisheni. Asante Bwana kwa ajili ya siku hiyo.

Kwa hiyo, wao, walikuwa huko chini kwenye vilima vya Yuda. Kulikuwa na M—Mtoto mchanga aliyezaliwa. Nyota ikatokea, na kadhalika.

Lakini baada ya siku nane, mama akamleta Mtoto mchanga, amevikwa nguo za kitoto. Ni nguo za kitoto. Ninasema … niliambiwa hiyo ilikuwa … Hawakuwa na kitu cha kumfunga. Ilikuwa kidogo ni—kidogo ni kijitambaa kilichotolewa kwenye nira ya maksai, nasikia, hicho ndicho kilikuwa ndio nguo Zake za kitoto. Huyu hapa Yusufu anakuja na hao wengine, akija pamoja na Mtoto huyu mchanga.

Ningewazia akina mama walisimama nyuma kwa mbali, wameshika watoto wao na mafulana na kila kitu. Kasema, "Angalia pale. Mnaona? Mnaona? Huyo hapo. Mnaona? Alikuwa amepewa mimba na mwanamume huyo. Huyu hapa anaingia. Hilo, kaa mbali naye. Kaa mbali." Wangali wanafikiria jambo lile lile.

Lakini, Mariamu, akiwa na Mtoto yule mchanga mikononi mwake, hakujali walivyodhani. Alijua huyo alikuwa ni Mwana wa nani.

51 Na ndivyo ilivyo kwa kila mwamini anayelikubali Neno la Mungu moyoni mwake! Sijali mifumo inasemaje. Mnajua ni kitu gani. Ni ahadi ya Mungu. Ilifunuliwa kwako na Roho Mtakatifu, wakati ulipofunikwa na Nguvu Zake. Unajua mahali ulipo. Hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri Injili mpaka amekutana na Mungu kule nyuma upande wa nyuma wa jangwa katika kile kijiti kinachowaka moto, ambako hakuna shirika la kidini ulimwenguni linaloweza kukuondolea Hilo. Ulikuwa kule. Lilitukia kwako. Sijali mifumo inasemaje. Wewe ni shahidi wa jambo hilo. Haleluya! Ninajisikia kama yule mzee mweusi niliyekuwa nikinena habari zake, "Sina nafasi hapa juu sasa." Mnaona? Ninajisikia wa kidini sana wakati huu, ninapowazia. Na hiyo ni kweli. Mungu, Mwenyewe, amekufunulia.

52 Simeoni alikuwa na ahadi. Akiketi kwenye chumba chake cha kusomea asubuhi hiyo, loo, nadhani huenda kukawa na watoto mia kadhaa walioletwa, kila asubuhi. Karibu Wayahudi milioni mbili na nusu nchini, na watoto hawa wachanga wanaingia, na wengi wanazaliwa. Kila baada ya siku nane ilimbidi mama huyo kuja, kutoa sadaka kwa ajili ya utakaso. Na sasa huyu hapa anakuja … Simeoni, ameketi

pale, mwajua, labda akisoma gombo la Isaya. Sijui. Lakini mara moja …

Sasa, kama Roho Mtakatifu amekupa ahadi, Roho Mtakatifu hana budi kutimiza ahadi hiyo, kama kweli ni Mungu. Yeye, kama Yeye …

Kama mtu akija na kusema jambo fulani, Mungu haungi mkono hilo, kwanza si Maandiko. Sahau. Na kama akisema ni kweli, na Mungu bado haungi mkono hilo, bado ni kosa.

Maana, Mungu anafasiri Ujumbe Wake. Yeye Ndiye anayejifasiria. Yale anayosema yanatimia, ndipo Mungu akasema, "Msikieni, kwa kuwa ni Kweli." Hiyo ni busara tu. Kama akisema litatukia, na linatukia, hilo linalidhihirisha. Haina budi kuwa ni kila wakati, Kweli kabisa, kwa sababu Mungu hasemi uongo.

53 Na kwa hiyo basi huyu hapa Simeoni ameketi pale, akistahimili mateso. Yeye alikuwa ndiye masalia. Alikuwa amemsikia Yohana, na masalia wachache wa siku hiyo. Na hapa alikuwa ameketi pale, akisikiliza gombo hili, akijua. Ninamaanisha, nikijua ya kwamba Yohana alikuwa anakuja, maana yeye—yeye alikuwa ni sehemu ya waliosalia. Alifunuliwa Neno. Na mara moja, wakati yule Mtoto mchanga alipoingia hekaluni, basi ilikuwa ni wajibu wa Roho Mtakatifu kufunua ya kwamba alikuwa pale. Kwa hiyo yeye, akiongozwa na Roho, akatoka kwenye kile chumba kidogo cha kusomea, moja kwa moja kupitia kwenye ule ukumbi, akafika kwenye mstari huo wa wanawake. Akaja moja kwa moja akifuata mstari huo wa wanawake mpaka akafika mahali alipokuwa huyu Mtoto Mchanga, wote walikuwa wanamuepa. Akamchukua yule Mtoto mchanga mikononi mwake, akasema, "Bwana, jalia mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako."

Na kwenye wakati huo, mwingine wa hao wachache walioteuliwa katika siku hiyo, alikuwa ni Ana, nabii mke. Alikuwa ameketi pale, kipofu, pembeni. Aliinuliwa, kipofu. Huyu hapa anakuja, akiongozwa na Roho, miongoni mwa wanawake wote na watu wanaosongamana ndani na nje ya hekalu, mpaka akaja moja kwa moja mahali ambapo Kristo Mtoto alikuwa.

Kama Roho Mtakatifu angeweza kumwongoza mwanamke kipofu Kwake, vipi kuhusu kundi la Kipentekoste linalopaswa kuwa na macho? Sitaenda mbele zaidi. Mnajua, tangu hapo na kuendelea. Angalia. Loo, jamani! Jinsi ambavyo kanisa hilo halina budi kuwa katika mchafuko wa kutisha tena, hakika halina budi kuwa, katika siku hiyo! Lakini liliwatikisa maskini mabaki, kama nilivyosema.

54 Sasa hebu na tuwe waaminifu. Kama tukiona kanisa hilo likiwa katika hali hiyo leo, si tumefikia wakati huo tena? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa angalia tu mambo ya ahadi, ya Biblia, ambayo yangekuwa yakiendelea kanisani wakati huu. Tunaona kinachoendelea ulimwenguni, na tunaona kiko mwishoni mwake. Sasa hebu na tuangalie kanisani.

Hilo, kanisa, lilipata utungu wa kuzaa chini ya Luther. Sasa, tunajua kuna nyakati saba za kanisa, na wajumbe saba kwa hizo nyakati za kanisa, kulingana na Ufunuo. Sasa, wakati ilipobidi Luther aje, bila shaka hilo lilitupa kanisa katika utungu wa kuzaa, lakini lilimzaa Luther. Hiyo ni kweli.

Baada ya hayo, lilipata shida tena, kwa hiyo likazaa Wesley. Hiyo ni kweli.

Likatoka tena, nalo likazaa pentekoste.

Kila mmoja wa hao wajumbe wa wakati wao, walitikisa … kurudi kwenye Neno, Ujumbe wa wakati wao, Ujumbe wa kulingana na Biblia. Nina kitabu kinachokuja, juu ya jambo hilo, ufafanuzi wa sura nne za kwanza za Ufunuo. Lisome, mara tu tutakapolipata kwenye magazeti. Na inathibitisha, bila shaka yo yote, ujumbe wa Luther ulikuwa nini, kuhesabiwa haki; utakaso ni nini, utaratibu unaofuata katika kuzaliwa kwa kawaida. Na ndipo wakaja wapentekoste, hasa.

55 Sasa, angalia, kila wakati ulilitikisa kanisa na kulipatia utungu wa kuzaa. Lakini walifanya nini? Baada ya utungu wa kuzaa kuja, badala ya kuendelea na Neno, walikusanya kundi la watu pamoja kama yule wa kwanza alivyofanya. Ni kweli kabisa. Mara baada ya mitikisiko ya mitume, ndipo tunamwona akienda zake tena. Ndipo tunaona ya kwamba moja kwa moja wakaja wengi wa hao wengine, Agabo na wengi wa wale watengenezaji huko nyuma katika mwanzo. Kila wakati ulikuwa umefanya hivyo, kama ukisoma kipindi kilichotangulia Baraza la Nikea, Waanzilishi wa Nikea, na huko nyuma kote. Unayapata yote mle ndani. Kila wakati ulitikiswa, kila wakati mjumbe alipotokea akiwa na BWANA ASEMA HIVI.

Sasa liko mahali pabaya sana, ambapo, kulingana na Maandiko, kwamba limewahi kuwa hivyo. Tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia, "Wakati wa kanisa tajiri, lakini uliopofushwa, ambao hawaujui."

Hakuna mahali popote katika Biblia ambapo Kristo alipata kufukuzwa kanisani, ila wakati wa Laodikia. Liko katika wakati mbaya sana. Limeoza sana kuliko lilivyopata kuoza. Kasema, "Nimeketi kama malkia, sina haja ya kitu."

"Wala hujui ya kwamba wewe ni uchi, mwenye mashaka, kipofu, maskini, wala hujui." Naam, bwana. Kasema, "Ninakushauri, njoo ununue dawa ya macho Kwangu, nipate kuyafumbua macho yako." Na hilo lita—hilo hakika … Dawa ya Mungu ya macho bila shaka italeta Nuru kwa kanisa kama linataka kufungua

macho yake kwa yale Mungu aliyosema.

56 Angalia, upesi sasa. Sasa, yeye yuko katika hatua hiyo, bila shaka. Tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia.

Sasa, mjumbe Wake ameahidiwa, katika Malaki mlango wa 4. Yeye ameahidiwa kufanya hivyo. Na Ujumbe ni kurudisha Neno, kuwarudisha watu kwenye Neno. Kuzaliwa kutakuweko. Litakombolewa, kwa Kuzaliwa upya, kulingana na Malaki 4.

Katika ulimwengu wa kanisa siku hizi, kuna mifumo miwili inayofanya kazi. Sasa sikilizeni kwa makini sana. Sasa nataka kuona kama utasema "amina" juu ya jambo hili. Kuna mifumo miwili inayofanya kazi katika ulimwengu wa kanisa siku hizi. Nitaondoa hili mabegani mwangu, halafu nitamalizia. Sote tunajua ya kwamba hilo ni Neno la Mungu, na mfumo wa kimadhehebu. Kuna mifumo miwili inayofanya kazi. Kama tu walivyokuwa, Yakobo na Esau; mmoja kutokana na Roho, huyo mwingine kutokana na mwili. Na ni kitu gani? Esau na Yakobo walikuwa wakipigana katika tumbo la uzazi la mama, hata wakati walipozaliwa. Na vivyo hivyo na madhehebu na Neno, wakipigana, mmoja dhidi ya mwingine. Wamekuwa hivyo, tangu Luther alipoleta matengenezo ya kwanza. Natumaini hilo ni rahisi vya kutosha hata mnaweza kulielewa. Mnaona?

Watu hawa, kama wakichukua *Hili* na kutoka pamoja Nalo, wanaweza kulifahamu zaidi, mnaona, kulifikisha mahali mngeweza. Ninataka tu kuweka Mbegu hii, kisha ninatumaini wataifanya iwe Uhai. Angalia. Mnaona?

57 Imekuwa hivyo daima. Hiyo ndiyo sababu linapata utungu wa kuzaa, kwa sababu kuna vita ndani yake.

Kuna Esau, mtu wa ulimwengu tu, wa kidini sana. Na, loo, yeye ni sawa, jamaa mwema, msafi, mwadilifu, kadiri nijuavyo mimi, bali yeye hajui kitu juu ya Haki hiyo ya Mzaliwa wa Kwanza. Amezaliwa hivyo. Yeye ameumbwa hivyo.

Na Yakobo, sijali yeye ni nani, yeye anataka hiyo Haki ya mzaliwa wa kwanza. Yeye ni wa kiroho.

Na hao wawili, leo, wako katika tumbo la uzazi la kanisa. Kuna mfumo mkubwa sana unaojaribu kuundwa, unaoitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na kutoka kwenye tumbo la uzazi la kanisa wanakuja watoto wawili. Wewe angalia tu neno langu. Ulimwengu …

Neno halina budi kulikomboa Kanisa Bibi-arusi Neno. Kanisa halina budi kuzaliwa kutoka kwake, Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo. Hao waliolala katika nyakati zote watamkamilisha huyo Bibi-arusi aliyetoka kwenye Neno walilotoka kwalo, kama vile kutoka kwenye miguu yako hadi kichwani mwako. Anakuwa—anakuwa mkubwa zaidi, na inakubidi kuwa na vya zaidi, na kadhalika. Kama vile mwili unavyokua, vivyo hivyo na Mwili wa Kristo unakua. Na halafu hatimaye Kichwa kitakuja Kwake, Kichwa Chake kitafanya hivyo, sasa, kama tukiangalia, maana Yote—Yote yameunganishwa na Kichwa. Kichwa hufanya kugeuka, kuvuta.

58 Lakini mifumo hii haitakua kutoka kwa Hilo, maana ni mfumo, wala hauwezi kuzaa. Gugu haliwezi kuzaa lundo la ngano. Lakini wote wawili wako kwenye shamba lile lile, wakimwagiliwa maji yale yale, na nuru ile ile ya jua. Moja ni Neno; moja si Neno. Na hao wawili wanapigana. Wamekuwa wakipigana tangu matengenezo ya kwanza, na wangali wanapigana.

Sasa, si lazima niendelee zaidi na jambo hilo, sivyo? Hakika mnajua ninalozungumzia. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Naam, bwana. Tuko hapo. Haya basi, mfumo. Uko katika mfumo gani?

Hebu wazia tu sasa, kama ungaliishi huko nyuma katika siku hizo, chini ya kufurahi kwa manabii wa Mungu na Maneno yaliyotokea, ungetaka kuwa upande gani huko nyuma?

Vema, una chaguo lile lile leo. Yeye anajiandaa kuleta Neno kamilifu nyuma kule, nalo Neno linakuja kwa ajili ya Bibi-arusi Neno. Kama vile mwa—mwanamke alivyo sehemu ya mwanamume, iliyoondolewa kwake, ndivyo Kanisa litakavyokuwa Kanisa linalotii Neno, kila Neno la Biblia; si taratibu, mafundisho ya sharti, wala chochote kilichoongezwa Kwake. Itabidi iwe katika Neno lisiloghoshiwa, safi, la bikira. Sawa.

Na katika siku za Nuru ya Luther, wakati bolti ya kanisa ilipofungwa, nguvu za Luther. Likaingia katika utungu, lakini yeye akatoka na, "Wenye haki wataishi kwa imani. Na *huu* si ushirika."

Sasa, tunaona, ya kwamba, chini ya siku za John Wesley, lilipatwa na uchungu tena, bali kulikuwako—kulikuwako na Wesley aliyezaliwa. Lakini alifanya nini? Akarudi moja kwa moja kama mama yake alivyofanya.

Ndipo chini ya siku za wapentekoste, baba zenu na mama zenu walitoka kwenye kitu hicho na kukichukia. Walitoka wakaenda mitaani, mama yako akiwa hana stokingi, akipiga-piga mkebe wa kale, na kuzungumza juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na gita la kale. Walilala kwenye barabara za magari,

wakalala gerezani usiku kucha. Nasi tumekomaa sana, na tumerudi moja kwa moja kwenye madhehebu na kujifanyia uchafu ule ule. Waliwavuta watoto wao wakawarudisha kwenye kitu kile kile walichotoka kwake. Wangeshikwa na hamaki kwenye makaburi yao. Wangekuonea aibu. Ninajua hilo ni gumu, bali ni Kweli. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

59 Unasema, "Nilidhani uliwapenda watu." Kama upendo hausahihishi, basi unawezaje kuzaa upendo? Upendo husahihisha. Nami naupenda ulimwengu … Nina—nina juhudi juu ya kanisa la Mungu.

Na kuona taratibu hizi zinazolifunga chini ya mafundisho ya sharti, zikioza. Na Mungu akitangaza Neno Lake kuwa ni Kweli, na bado wanalishikilia. Amina. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hiyo ni kweli. Unajua ni kweli, ndugu, dada. ["Amina."] Hilo ni Hili tu. Hiyo ndiyo njia rahisi ya kulielezea. Si—si swala la kuchambua Kiyunani, na kadhalika, lakini ni kuvunja-vunja na kuonyesha maana ya kwawaida. Hakika unaweza kufahamu Hilo. Mbili na mbili ni nne. Mnaona? Sasa tunajua ya kwamba hiyo ni kweli.

Sasa, Neno halina budi kumzaa Bibi-arusi.

60 Lakini ule mfumo wa kale hauna budi kuweka mfano wake. Haina budi kumzaa Esau aliyeuza haki zake za mzaliwa wa kwanza.

Hili hapa linakuja. Ninalihisi. Natumaini hamfikiri mimi ni mwenda wazimu. Vema, kama ndivyo nilivyo, niache. Ninajisikia vizuri hivi. Mimi ni bora zaidi hivi kuliko nilivyokuwa upande ule mwingine. Ni—huenda nikawa mwenda wazimu, kwa ulimwengu. Ni—ni—ninajua mahali nilipo. Ninajua mahali ninaposimama.

Angalia. Utazaa mtoto mfu, shirika la kidini litakaloyakusanya madhehebu yote pamoja, kumzaa Esau fulani anayemchukia Yakobo. Amina. Natumaini mnaliona, dhehebu lililokufa, lililokufa, yote yakiungana pamoja.

Loo, enyi waaminio wa Neno, toeni Ujumbe wangu. Nisikilizeni, si Ujumbe wangu, bali Ujumbe Wake ambao Yeye anautangaza dhahiri kuwa ni Kweli. Huna budi kuchagua kutoka mahali fulani. Huwezi kukaa kimya baada ya jambo hili. Huna budi kufanya chaguo lako.

61 Mnakumbuka hivi majuzi, huko Westward Ho kule, kwenye asubuhi hiyo, kwenye kiamshakinywa hicho, jinsi Bwana alivyoniruhusu niwaonyesheni hiyo ngano? Jinsi ilivyochipuka kupitia kwa Luther, kupitia kwa Wesley, na vishada, na kadhalika, na vitawi vidogo vilivyojitokeza, kila kanisa limewakilishwa katika ghala ya mahindi. Ndipo ikashuka ikaingia moja kwa moja kwenye hiyo ngano, kama ilivyokuwa, na kulikuwako na hilo kapi dogo, lililifanana kabisa na punje halisi ya ngano. Unapotoka na kuangalia, kama hujui ngano yako, utasema una ngano pale, bali ni kapi tu. Ndipo unafungua hilo kapi, hakuna ngano pale, hata kidogo. Huko nyuma kabisa, kuna chipukizi dogo la uhai linalokuja. Unachukua glasi na kuiangalia. Na wakati Pentekoste ilipotokea mara ya kwanza, ilikuwa imekaribia sana, Yesu alisema katika Mathayo 24:24, "Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Ilikuwa ni kufanya nini? Msaada wa punje. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa, kishada …

Angalia hapa. Hilo jani halifanani na punje iliyoanguka, wala kishada, lakini hufanana zaidi Nayo. Na kapi linafanana sana nayo, bali hata hivyo si ngano. Ni mbebaji wa ngano.

62 Hivi hamwoni jinsi jumbe hizo zimekuja na maumivu ya uzazi? Bali Uzima uliachwa moja kwa moja kutoka pale, kwenda kwenye ujumbe unaofuata. Uzima huo ulitoka moja kwa moja kutoka kwa Luther, ukaingia katika ujumbe wa Wesley. Moja kwa moja kutoka kwenye ujumbe wa Wesley, ukaingia kwenye ujumbe wa kipentekoste. Sasa wakati umewadia tena, kuondoka kwenye kapi. Kuna nini? Kuna maumbile, katika kila namna, yakitangaza kwamba hiyo ni Kweli.

Sasa mnaona ni kwa nini unafikiri mimi ni mwenda wazimu. Labda ndivyo nilivyo, kama nilivyosema. Lakini kuna Kitu fulani ndani yangu. Siwezi kukizuia. Kamwe sikukiweka pale. Hakikuja kwa kuchagua kwangu. Ni Mungu. Naye hukithibitisha, kukihakikisha ya kwamba ni Kweli, kukifanya Kweli. Si kwamba nina jambo lo lote dhidi ya Luther, na Wesley, Wapentekoste, ama Wabaptisti, ama yeyote yule. Hakuna kitu dhidi ya mtu ye yote. Mifumo hiyo ndiyo ninayopinga, kwa sababu Neno linaipinga; si watu. Waangalie hawa makuhani na makasisi wanaoketi hapa, leo. Wasingekuwa hapa kama wangalisikiliza mfumo, bali walikuwa na ujasiri wa kawaida, wa Neno la Mungu, kutoka na kulikubali. *Haleluya* maana yake ni "Mungu wetu asifiwe." Halitawadhuru. [Mtu fulani anasema, "Amina." — Mh.] Inamaanisha "na iwe hivyo." Ninaamini jambo Hilo. Ninaamini na ninajua ya kwamba ni Kweli. Imethibitishwa kuwa ni Kweli. Siku moja utaona, labda umechelewa sana. Sasa angalia. Angalia.

63 Biblia ilisema, "Mkewe amejifanya tayari," mwishoni mwa wakati. Alijifanyaje tayari? Kufikia kuwa Mke Wake. Naye anafanya nini? Alikuwa amevaa vazi la namna gani? Neno Lake Mwenyewe. Alikuwa amevalia Haki Yake. Hivyo ndivyo ilivyo. Ni sahihi. Mnaona?

Maono! Angalia, tunafunga tu sasa. Ninataka kusema jambo hili moja kabla tu ya kufunga. Hilo ndilo lililonifanya niseme jambo hili. Sasa, ni BWANA ASEMA HIVI. Kama mtu angesema jambo hilo, bila, kuliweka katika mawazo yake mwenyewe, angekuwa mnafiki na anapaswa kwenda kuzimu kwa ajili yake.

Hiyo ni kweli. Kama angejaribu kupata kundi la watu, watu wazuri kama hawa, na kuwadanganya, mbona, angekuwa ni ibilisi katika mwili wa kibinadamu. Mungu kamwe asingemheshimu. Unafikiri Mungu angemheshimu shetani ama uongo? Kamwe. Mnaona? Linapitia juu ya vichwa vyao, nao hawalipati. Yeye huwavuta Wateule.

64 Waangalie manabii wote katika nyakati, jinsi alivyowapata Wateule.

Angalia, tukishuka kupitia, hata kwenye yale matengenezo. Kama vile, kanisa Katoliki la Kirumi lilimchoma moto Joan wa Arc, kwa kuwa ni mchawi. Hiyo ni kweli. Baadaye waligundua hakuwa. Alikuwa ni mtakatifu. Bila shaka, walifanya vitubio, wakaichimbua miili ya hao mapadre na kuitupa mtoni. Lakini, mnajua, lakini hilo halikutatua mambo katika vitabu vya Mungu. La. Walimwita Mtakatifu Patrick hivyo, pia, mnaona, na basi kama mimi ni mchawi yeye naye ni mchawi pia. Kwa hiyo, tunaona, angalia watoto wake. Angalia mahali pake, juu, angalia ni wangapi waliouawa. Angalia kwenye elimu ya wafia imani uone ni wangapi waliouawa pale. Mnaona, sivyo ilivyo.

Lakini madai ya watu, hilo halilifanyi kuwa hivyo. Ni yale Mungu aliyosema na kuthibitisha, kwamba ni Kweli. "Thibitisha mambo yote. Shikilia sana yaliyo mema."

65 Sasa tunaona, sasa, hapa yapata miezi michache iliyopita, asubuhi moja, nilikuwa nikitoka nje ya nyumba, na ono likaja.

Nami ninatoa changamoto kwa mtu ye yote hapa, ambaye amejua miaka hii yote, akaseme wakati wo wote ambapo Bwana aliwahi kuniambia "BWANA ASEMA HIVI" ila jambo hilo lilitukia. Ni wangapi wanaojua ni Kweli, inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sawa. Kuna mtu yeyote angeweza kunena kinyume? [Ndugu Branham anatulia. Kusanyiko liko kimya.] Ni kweli.

Usimsikilize mjumbe. Angalia Ujumbe ulivyo. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona? Si hivyo. Msichunguze maskini [Sehemu tupu kwenye kanda.] Mwenye upara, mwajua, mtu, maana ni—ni mwanadamu tu, wote, na sisi sote ni sawa tu. Lakini angalia kile kinachotendeka. Hilo ndilo linalotangaza jambo hilo. Nilichukuliwa …

Sasa, ninajua watu wanasema kila namna ya mambo, nasi tunajua ya kwamba mengi ya hayo si sahihi. Siwezi kujibu kwa yale mengine, mtu ye yote asemayo. Sina budi kujibu yale ninayosema. Ninaweza tu kusema kama ni Kweli, ama si Kweli. Na mimi—mimi—mimi ndiye ninayepaswa kuwajibika kwa jambo hilo, si yale mtu mwingine asemayo. Siwezi kumhukumu mtu ye yote. Sikutumwa kuhukumu, bali kuhubiri Ujumbe. Angalia.

66 Ilibidi nionyeshwe—nionyeshwe Kanisa. Nami nilichukuliwa na Mtu Ambaye sikuweza kumwona, nami niliwekwa juu, kama, stendi. Nami nikasikia muziki mtamu sana niliopata kusikia. Nami nikaangalia, likija, na kundi la mabibi wadogo, karibu, walionekana kuwa, loo, umri wa miaka kama ishirini, kumi na minane, ishirini. Nao wote walikuwa na nywele ndefu, na walikuwa wamevaa nguo mbalimbali, mfano, nguo. Nao walikuwa wakipiga hatua kwa hatua kamilifu, kwa muziki huo, kama ilivyoweza kuwa. Nao wakaenda kutoka kushoto kwangu, wakizunguka upande *huu*. Nami niliwaangalia. Ndipo nikaangalia basi kuona ni Nani aliyekuwa akizungumza nami, nami sikuweza kumwona mtu ye yote.

Ndipo nikasikia bendi ya roki ikija. Na wakati nilipotazama upande wangu wa kuume, nikija huku, nikirudi, haya hapa makanisa ya ulimwengu yanakuja. Na baadhi ya … Kila mmoja amebeba bendera yao, kutoka mahali walipotoka. Baadhi ya mambo yaliyo machafu sana niliyopata kuona maishani mwangu! Na wakati kanisa la Marekani lilipokuja, lilikuwa jambo baya sana nililopata kuona. Baba wa Mbinguni ndiye Hakimu wangu. Walikuwa wamevaa sketi hizi chafu sana za kijivu, kama mmoja wa hawa wasichana wa baa, zilizo tupu upande wa nyuma, hapa juu; wameshikilia kitu kinachoonekana kama kipande cha karatasi ya kijivu; na kama dansi la hula; wamejipaka rangi; wamevaa kaptura fupi, wamekata nywele; wanavuta sigara; na wakikatika viuno, huku wakitembea kwa mdundo wa roki.

Nami nikasema, "Hilo ni kanisa la Marekani?"

Nayo Sauti ikasema, "Naam, ndiyo."

67 Nao walipopita, iliwabidi kukishikilia namna *hii*, na kuiweka ile karatasi nyuma yao walipopita.

Ni—nilianza kulia. Ni—niliwazia tu, "Katika kazi yangu yote, na yote niliyofanya." Na kila kitu ambacho sisi wahudumu tumefanya kazi pamoja … Na, ndugu, si—sijui ni kiasi gani mngeamini juu ya maono haya; bali ni Kweli, kwangu mimi. Daima imethibitishwa kuwa ni kweli. Nilipoona jambo hilo, na nikijua kilichokuwa kikiendelea, moyo wangu ulikuwa karibu kupasuka ndani yangu. "Nimefanya nini? Nimelikosaje? Nimedumu moja kwa moja na Neno hilo, Bwana. Na ningewezaje kufanya jambo hilo?"

Niliwazia, "Ungewezaje Wewe kunipa ono, si muda mrefu uliopita, na kuniona Humo? Nami nikasema, 'Vema, je! Itawabidi kuhukumiwa?' Akasema, 'Kundi la Paulo, pia.' Nikasema, 'Nimehubiri Neno lile lile alilohubiri.'" Wafanyabiashara Wakristo walibeba makala yake. Nami nikasema, "Kwa nini? Kwa nini iwe

hivi?”

Niliona lile kundi la malaya likipita namna hiyo, wote wamevalia namna hiyo, na kujiita, “Kanisa la Bi Marekani.” Nilizimia tu.

68 Ndipo, moja kwa moja, nikasikia ule mziki mtamu halisi ukija tena, na huyu hapa Bibi-arusi mdogo yuaja tena. Yeye alisema, “Hiki ndicho kinachotoka, hata hivyo.” Na wakati alipopita pale, Yeye ni kama yule yule kwanza, akitembea kwenye hatua ya muziki wa Neno la Mungu, akipita mbele. Na nilipoona jambo hilo, nilisimama pale huku nimeinua mikono yangu miwili, nikilia, namna *hiyo*. Nilipokuja, nilikuwa nimesimama kwenye ukumbi wangu huko nje, nikiangalia moja kwa moja kote uwanjani.

Nini? Yeye anapaswa kuwa Bibi-arusi yule yule, wa aina ile ile, aliyejengwa kwa nyenzo ile ile aliyokuwa nayo kwanza. Sasa soma Malaki 4 uone kama hatupaswi kuwa na Ujumbe katika siku za mwisho, ambao “utaigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao,” kurudi kwenye Ujumbe wa asili wa kipentekoste, Neno kwa Neno. Ndugu, tuko hapa.

Sasa, kanisa hili linapaswa kupata ishara, na ishara yake ya mwisho. Tunaona hapa, katika—katika—katika Maandiko, unaona sasa, unaona, utungu mkuu wa kuzaa ambao uko katika wakati huu wa Laodikia. Inachosha. Kanisa lao linazaliwa mara ya pili. Si …

69 Hakutakuwako na dhehebu lingine kamwe. Kila mtu anajua ya kwamba kila wakati ujumbe ulipotolewa … Waulizeni hawa wanahistoria. Baada ya ujumbe kutolewa, dhehebu lilitoka kwake; loo, Alexander Campbell, kila kitu kingine, Martin Luther, na kila kitu. Waliunda madhehebu kutoka kwake. Na kwa kawaida ujumbe huenda tu kwa miaka mitatu hivi, uamsho. Hili limekuwa likitendeka kwa miaka kumi na mitano, na hakuna dhehebu lililotoka kwake. Kwa nini? Kapi lilikuwa ndilo la mwisho. Tuko mwishoni.

Mnaona utungu wa kuzaa? Mnaona kuna nini? Ni mabaki tu watakaotolewa. Ni mabaki tu watakaotolewa. Na hiyo ndiyo sababu ninalia, na kukazana, na kusukuma, na kuweka kando kila upendeleo wa mwanadamu duniani, kupata kibali kwa Mungu, na kuendelea tu katika Neno Lake.

Linaumwa. Hiyo ndiyo shida. Litazaa. Halina budi kufanya chaguo lake. Maandiko hayo yako ukutani. Tunaona dunia iko karibu kabisa kuondoka. Hiyo ni kweli. Nasi tunaona kanisa, limeoza sana, liko tayari kwenda. Na utungu wa kuzaa uko juu ya hayo yote, juu ya ulimwengu na kanisa pia.

Na kuna karibu kuzaliwa ulimwengu mpya, na Kanisa jipya kuzaliwa, kuuendea, kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Tunajua jambo hilo.

70 Angalia. Mungu humpa … Na sikilizeni kwa makini hili, ndipo ninafunga. Ishara yake ya mwisho; Ujumbe wake wa mwisho, ishara yake ya mwisho. Ishara yake ya mwisho, ni, hana budi kuingia katika hali kama ilivyokuwa hapo mwanzo; ulimwengu, kanisa.

Angalia jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo, miaka hiyo yote, bila, tangu Malaki mpaka Yesu. Liangalie, miaka yote sasa. Liangalie, huko nyuma kote, walivyoingia kwenye upotovu. Angalia nchi, jinsi ilivyokuwa kila wakati, kama katika siku za Nuhu, na kadhalika. Haina budi kuwa katika namna ile ile ya mfano, nasi tunaona jambo hilo. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Tunaona mambo haya yote yakifanana tu.

71 Halafu, tunapata ishara moja ya mwisho. Katika Luka, mlango wa 17, kifungu cha 28, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Kwa kuwa, kama ilivyokuwa Sodoma, mnaona. Sasa, Yesu alisoma Biblia hii hii, Mwanzo ule ule tunaousoma. Sasa, karibu, msilikose. Biblia ile ile tunayosoma, Yesu aliisoma. Naye aliliambia Kanisa Lake, “Angalia nyuma uone wakati siku za Sodoma zitakaporudi tena,” watu waliopotoka, watu wakipoteza maumbile yao ya kawaida.

Angalia ulawiti, jinsi unavyoongezeka ulimwenguni siku hizi, katika gazeti hivi karibuni tu. Mnapaswa kuingia ofisini mwangu na kusoma barua kutoka kwa mama, kwa ajili ya wavulana wao. Na ulawiti unaongezeka, nafikiri, ni asilimia ishirini ama thelathini katika—huko California, peke yake, mwaka jana. Kundi kubwa la … la hata watu wa serikali, limethibitisha kuwa wao ni walawiti. Ninyi watu wa serikali mnajua jambo hilo. Magazeti yenu, niliyasoma, na katika mambo mbalimbali yaliyotukia. Kama wewe …

[Dada fulani ananena kwa lugha nyingine, halafu anatoa tafsiri. Dada yule yule tena anazungumza kwa lugha nyingine, halafu tena anatoa tafsiri. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

72 Nina ufahamu sahihi wa Maandiko. Hilo ndilo hasa Mungu alilosema lingetukia. “Yeye anenaye kwa lugha na aombe apate kufasiri.”

Hiyo iwe kweli. Nimewaambia Kweli, basi Mungu yuko hapa, akilithibitisha. Ni Kweli. Hiyo ni kweli.

Sasa angalia. Ulikuwa ni Ujumbe gani wa mwisho ambao Yesu alisema? “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” sasa angalia, kabla tu ya ulimwengu wa Mataifa kuteketezwa, ule moto. Sasa jaribu kuelewa. Ni kitu gani kilichotukia? Kulikuwako na kundi la watu, washiriki vuguvugu wa kanisa, kama Lutu

na kundi lake kule Sodoma. Kulikuwako na mtu mwingine aliyekuwa tayari ametoka kwake. Yeye hakuwa ndani yake, kwanza. Huyo alikuwa ni Ibrahimu, yule aliyekuwa na ahadi ya kuja kwa mwana. Mnaelewa? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema.

Na, sasa, kabla tu ya kilele cha maangamizi kuja, Mungu alimtokea Ibrahimu katika namna nyingi, lakini wakati huu anaonekana kama Mwanadamu. Yeye alikuwa Mwanadamu. Naye akamjia Mungu.

Sasa, unasema, "Hakuwa Mwanadamu."

Ni—ni—ni—ni Mungu katika Mwanadamu. Ibrahimu alimwita, "Elohimu." Ilikuwa ni Mwanadamu.

Na, angalia, Yeye aliketi chini, ameelekeza mgongo Wake hemani, Naye akasema, "Yuko wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

Kasema, "Nitakuzuru wakati huu mwakani, ambapo nilikuahidi." Ndipo Sara akacheka. Naye akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Mnaona?

73 Sasa, hicho ndicho kilichokuwa kikiendelea katika siku hiyo. Kuonyesha tu ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona, kundi la Walioteuliwa likitolewa, kutoka Sodoma. Sasa, msikose mfano huu, chochote mfanyacho. Kundi lililokuwa limevutwa, ambalo halikuwa Sodoma, kwanza.

Lakini Malaika wawili walishuka wakaenda Sodoma. Na wakati walipofika kule chini, tunamwona Lutu. Naye akamkuta katika hali ya kurudi nyuma, mashoga wote na upotovu. Mnajua hadithi hiyo.

Lakini kuna Mmoja aliyebaki na Ibrahimu, alikuwa ni Elohimu.

Walihubiri Neno kule chini. Kuhubiri Neno kuliwapofusha, nao hawakuweza kupata mlango. Hivyo ndivyo ilivyo leo.

Lakini Yule aliyekuwa pamoja na kundi lililotoka, alifanya muujiza mbele ya Ibrahimu, kuonyesha kwamba yeye alikuwa ni nani, naye alikuwa pamoja na Ibrahimu.

Akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" kuhusu mtoto huyu. Ndipo Sara akajitokeza na kusema hakufanya hivyo. Kisha akasema, "Lakini ulicheka." Naye angemwua papo hapo kama yeye hakuwa ni sehemu ya Ibrahimu.

Vivyo hivyo Mungu angetuua kama hatukuwa sehemu ya Kristo. Rehema ya Kristo yote inatushikilia pamoja, sisi wenye kushuku na upotovu katika Neno.

74 Lakini, angalia, angalia kilichotukia. Yesu anageuka nyuma sasa, na kusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa mwisho wakati Mwana wa Adamu atakapoanza kujifunua Mwenyewe." [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Mnaona? "Mwana wa Adamu" daima, katika Biblia, ni *nabii*. Mnaona? Yeye alikuja katika Jina la wana watatu: Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Mnaona? Naye alitamka Jina Lake, "Mwana wa Adamu," kwa sababu hiyo ndiyo kazi aliyofanya, ya nabii, mwonaji. Yeye alisema, "Katika siku kama ilivyokuwa katika Nuhu, wakati Mwana wa Adamu atakapoanza kujifunua Mwenyewe, huo utakuwa ni wakati wa mwisho."

75 Sasa hebu na tuwazie, kwa dakika moja tu. Kamwe ulimwengu haujapata kuwa na mjumbe juu ya ulimwengu. Tumekuwa na akina Finney, Sankey, Moody, Finny, Knox, Kalvini, na kadhalika, kote ulimwenguni, wajumbe kwa kanisa katika utungu huu wa kuzaa. Lakini kamwe hatukuwahi kuwa na mtu anayetoka na ujumbe wa kimataifa, mpaka siku hii, jina lake likiishia katika h-a-m. A-b-r-a-h-a-m, ambayo ni herufi sita … A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba.

Tuna moja leo inayoitwa G-r-a-h-a-m, herufi sita, na sita ni namba ya ulimwengu, siku ya uumbaji. Ni lini ulimwengu ulipata kuwa na mtu ndani yake sasa, akihubiri katika ulimwengu, kule ulimwenguni, kule chini akiwaita watu watoke, "Tubuni, tubuni!, Mtaangamia, iwapo hamtatoka kwake," mpaka wakati huu? G-r-a-h-a-m, angalia kile anachofanya, akihubiri Neno, akiwapofusha watu wa nje, akiita, "Tokeni," mjumbe kutoka kwa Mungu. Yesu alisema hilo lingetukia wakati tu Mwana wa Adamu atakapojifunua Mwenyewe. Sasa, hilo, hilo liko wapi? Huko nje katika taratibu za kanisa, ulimwenguni. Nao wakaanza kumchukia mtu huyo, kwa ajili ya jambo hilo.

76 Lakini, kumbukeni, kulikuwako na kundi, pia, hilo lilikuwa ni kundi la kiroho, kundi la Yakobo, si—si kundi la Esau. Kuna kundi la Yakobo lililokuwa likimtafuta mwana, ambalo halikuwa katika ile Babeli, nao wakampokea Mjumbe. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."- Mh.] Ibrahimu, A-b-r-a-h-a-m, wao walimpokea Mjumbe. Na huyo Mjumbe, ni jambo gani kuu, la ajabu alilofanya, kuonyesha ilikuwa katika wakati wa mwisho? Yeye alitambua mawazo yaliyokuwa katika mawazo ya Sara.

Na Yesu, Mwana wa Mungu, ambaye alifanyika mwili, akionyesha ya kwamba Roho wa Mungu angeshuka chini katika lile kundi dogo lililoteuliwa la wakati wa mwisho, na angejifunua Mwenyewe katika

njia ile ile. Utungu wa kuzaa! Loo, ndugu, tafadhali jaribu kuelewa. Jaribu sana. Fungueni mioyo yenu kwa dakika moja. Mtazame Kristo. Mungu huyo huyo yuko papa hapa sasa. Yeye yule. Yeye aliahidi mambo haya. Na kama Yeye aliwaahidi, hakika Yeye anaweza kuyafanya.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Ninawatakeni mfikirie tu, kwa uchaji.

77 Baba, liko mikononi Mwako sasa. Nilifanya yote niwezayo kufanya. Ninaomba ya kwamba utawasaidia watu ku—kufahamu. Mbegu imepandwa. Mimina maji, Roho, juu Yake, Bwana, na uimwagilie maji kwa ajili ya utukufu Wako. Kama nilifanya kosa, Bwana, sikukusudia kufanya hivyo. Ninaomba, Mungu, ya kwamba —ya kwamba utalifasiri vizuri, mioyoni mwao, wapate kuona na kufahamu. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

Bwana awabariki. Ninawapenda. Mungu huyu aliyehubiri Neno hili, Mungu huyu anayewajibika kwa Neno hili … Ninawajibika tu kulisema. Yeye ndiye anayepaswa kulihuisha. Mungu huyo huyo yupo hapa.

Sasa, ni wangapi huko nje walio na haja? Inua mkono wako. Je! Yeye aliahidi kufanya mambo haya katika siku za mwisho? Sasa niangalieni mimi. Sasa ni kama Petro na Yohana walivyosema, "Tuangalie." Kama kwamba … Mnaona? Akamwambia. Sasa angalia upande huu. Sasa, tafadhali msisogee. Hili ni ninii sana … Nina—ninajaribu, moyo wangu wote ndani yangu. Iweni tu na kicho sana. Mnaona? Kila mmoja wenu, ni roho, mnaposogea. Bila shaka, wewe ni kitu kimoja. Ninajaribu kushika imani ya hawa watu.

Maskini mwanamke mmoja akapita na kugusa vazi Lake, akatoka akaenda akaketi. Yesu alimwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akaponywa.

Na sasa Yeye aliahidi kufanya jambo hilo tena, Mwana wa Adamu angejifunua Mwenyewe kama alivyofanya huko Sodoma. Ulimwengu uko katika hali hiyo. Kanisa liko katika hali hiyo. Sasa je! Mungu ametimiza Neno Lake? Angalia kama amelitimiza, ama hajalitimiza. Loo, tumekuwa na ishara, kuruka, kunena kwa lugha, unabii, na kadhalika. Lakini, ngoja, kuna ishara nyingine. Loo, tuna uigaji mwingi wa kimwili. Hilo linamfanya yule wa kweli kung'aa. Dola yo yote ya bandia inapaswa kuifanya ile ya kweli kung'aa.

78 Sasa ombeni. Mnaamini. Ni kwamba tu, ni—ninawapa changamoto kufanya jambo hilo. Angalia, namwuamini yale niliwaambia. Ni wangapi wanaamini hii kuwa ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." —Mh.] Jali wewe ni nani, uko wapi. Nitaninii tu …

Kila mtu humu ndani, kadiri nijuavyo mimi, ni mgeni kabisa, isipokuwa Bill Dauch na mkewe wameketi papo hapo, nijuavyo mimi. Nafikiri ninamjua maskini mhubiri huyu hapa kutoka Ujerumani, anayeketi pale. Na, ndugu, na watu wawili ama watatu wameketi papo hapo.

Mtu fulani huko nyuma katika wasikilizaji, angalieni, huko nyuma kabisa. Ninawahimiza kuamini yale niliyowaambia ni Kweli.

Vipi kuhusu wakati yule Malaika wa Bwana aliposhuka mtoni kule, miaka thelathini na mitatu iliyopita, na kutoa tamshi hili? Nilijuaje?

Na mchungaji wangu wa Kibaptisti alinifukuza kanisani, kasema, "U—ulikuwa na jinamizi, Billy."

Nikasema, "Jinamizi, hata kidogo, Dk. Davis. Hivyo ndivyo wewe, msimamo unaochukua, hata afadhali uchukue kadi yangu ya ushirika."

Nilijua kungekuwako na mtu fulani, mahali fulani, angeamini jambo Hilo. Mungu hangetuma Ujumbe kusiwe na watu wa kuupokea.

Loo, hakika, nilipoenda kuwaombea wagonjwa, ilikuwa ni vizuri sana. Lakini wakati ninapoanza kuwaambia Kweli ya Neno, basi ni tofauti. Mnapaswa kujua. Kila Ujumbe umekuwa hivyo.

79 Yesu alikuwa mzuri sana alipoenda kanisani na kuwaponya watu, na kila kitu. Lakini wakati alipoketi chini siku moja, na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja," loo, hilo, hilo lilitosha. "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu." Yeye hakulielezea. Alitaka kuona ni nani atakayesimama karibu Naye. Sawa.

Unafikiri nini, m—umati wenye madaktari na kadhalika, unasema, "Mtu huyo ni … Mbona, Yeye ni kizuu mfyonza damu. Kula mwili Wake na kuinywa Damu Yake?" Yeye hakulielezea kamwe. Yeye hakulielezea kamwe.

Lakini, hata hivyo, Neno hilo lilikuwa likishikilia, kwa hao mitume. Hawakujali. Hawakulifahamu. Waliliamini, hata hivyo. Mnaona? Walijua, maana walikuwa wameona kazi za Mungu, nao walijua ilikuwa hivyo. Yeye alisema, "Hao ndio wanaonishuhudia Mimi."

80 Huyu hapa mwanamume, mwanamke ameketi papa hapa, ameinua mkono wake. Sasa, mnaweza kuniita mshupavu wa dini, ukitaka; bali Nguzo ile ile ya Moto, iliyowaongoza wana wa Israeli kupitia

jangwani, iko moja kwa moja juu ya mwanamke huyo.

Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona. Nimetoka kwa Mungu. Ninaenda kwa Mungu," baada ya kifo Chake, kuzikwa. Aliwaambia Wayahudi. Yeye alisema, "Mimi …"

Yeye alikuwa ndiye ule Mwamba uliokuwa nyikani. Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO." Ni Nani aliyekuwa "MIMI NIKO"? Ile Nguzo ya Moto katika kile kijiti kilichowaka moto. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Naye alifanyika mwili akakaa kwetu. Kasema, "Nilitoka kwa Mungu, na kumrudia Mungu, kusudi nirudi katika umbo la Roho Mtakatifu."

Na Ndiye huyu hapa, pamoja nasi leo, picha Zake za kisayansi. Huyu hapa, kuthibitisha zaidi ya picha yo yote ya kisayansi, chochote kile. Yeye yuko hapa, kuthibitisha jambo hilo, kwa kuwa ni Yeye. "Mimi Mwana wa Adamu nitafunuliwa katika siku hii." Sasa, *yule* pale. Ninamtazama moja kwa moja.

Unasema, "Je! Unaiona?" Yohana aliiona, pia, lakini hao wengine hawakuiona.

81 Angalia, kulithibitisha hilo sasa. Mwanamke huyo ni mgeni kwangu. Sijawahi kumwona—yeye, maishani mwangu. Lakini ana kasoro fulani katika mojawapo ya viungo vyake ambavyo anaombea. Ni … Hiyo ni kweli, mama. Ulifanyiwa upasuaji. Huyo ni mume wako anayeketi karibu nawe. Wewe hutoki hapa. Umetoka California. Jina lako ni Roland. Shida yako ya tumbo imeisha, pia, bwana. Ulikuwa na ugonjwa wa tumbo. Sivyo? Vema, yote yamekwisha. Mguu wako umepona.

"Katika siku hiyo Mwana wa Adamu …"

Hapa, ameketi moja kwa moja kupitia *hapa*, kuna mtu. Yeye ni mtu mweusi, ana kasoro kwa macho yake. Yeye ni ninii … Ndiyo. Yeye, kazi afanyayo, yeye hufanya jambo fulani kuhusu motokaa, huosha motokaa, mwosha magari. Sawa. Macho yako yanaenda kombo. Ndiyo kwanza uamini, sivyo? Jambo fulani la ajabu sana lilikupata. Jina lako la kwanza ni Fred. Hiyo ni kweli. Jina lako la mwisho ni Conn. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa? Macho yako hayatakusumbua tena basi. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu.

82 Mtu huyo aliye nyuma moja kwa moja kule nyuma, yeye pia hatoki hapa. Kutoka California. Una mgongo mbaya, Bw. Owens. Huyo ni wewe. Bwana Yesu akuponye. Sijapata kumwona mtu huyo, maishani mwangu, sijui kitu kumhusu. Mimi ninaifuata tu hiyo Nuru inavyoenda.

"Kama mnaweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio."

Jamaa mdogo anayeketi hapa, ana ngiri, amevaa miwani na suti ya kijivu. Fred, Mungu anakuponya kama unaamini. Utakubali jambo hilo? Vema. Sijapata kumwona, maishani mwangu.

Bibi Holden, unayeketi kule kutoka kwake, unayeumwa na macho. Simjui mwanamke huyo, sijapata kumwona maishani mwangu, bali hiyo ni kweli. Mnaona? "Kama unaweza kuamini."

Unalia nini, dada? Una ugonjwa wa kuchanganyikiwa, vidonda kooni, ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unayeketi mwishoni mwa kiti pale. Kama unaamini, kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Wasiwasi huo wote utakuacha, unajisikia kana kwamba umerudi katika hali yako njema. Ibilisi anakudanganya. Mnalikubali? Sasa inua mkono wako, useme, "Nitakubali, basi." Sawa. Yote yamekwisha.

83 Nini? Kanisa hili linapitia katika utungu wa kuzaa. Hivi hutafanya chaguo lako sasa katika Uwepo Wake? Nimewaonyesha Neno hasa, yale aliyosema angefanya.

Tafuteni kwenye jengo hili, mwulizeni mtu ye yote aliyewahi kuguswa, ama kuzungumziwa, ama cho chote kile kilichofanyika, na mwone kama nimewahi kuwaona, kuwajua, ama jambo lolote juu yao. Mnafikiri mwanadamu angeweza kufanya jambo hilo? Hilo haliwezekani kabisa kwa jambo hilo kutukia.

Vema, ni Kitu gani? Mwana adamu. "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili, likitambua roho, siri za mioyo." Ni kama tu vile lilivyokuwa kabisa wakati lilipofanyika mwili hapa duniani, katika Mwana wa Mungu, sasa linafunuliwa na Mwana wa Mungu kwani Yeye amekuja kumwita Bibi-arusi kutoka kwenye mfumo huo. "Tokeni kwake. Mkatengwe, asema Mungu. Msiguse vitu vyao vichafu, na Mungu atawapokea."

Je! Uko tayari kuyatoa maisha yako yote kwa Mungu? Kama uko tayari, simama kwa miguu yako, useme, "Nitalikubali, kwa neema ya Mungu, sasa hivi, kwa kila kitu kilicho ndani yangu."

84 Haleluya! Mungu asifiwe! Unamwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Basi inua tu mikono yako na uombe pamoja nami.

Ungama makosa yako. Utungu wa kuzaa! Ni vigumu kufa, bali kufa sasa hivi. Kufa, toka kwenye imani yako ya kutokuamini. Tokeni kwake. Hili ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, kama tu lilivyokuwa wakati

Yesu alipokuja duniani. Ni Yesu Kristo tena miongoni mwenu, aliyethibitishwa.

Ibrahimu alipokea mwana mara moja, mwana aliyeahidiwa, baada ya jambo hilo kutukia.

Na Yesu anakuja tena. Huyo ni Roho Wake. Yeye yuko karibu sana na dunia, yuko karibu sana kuja, hata yuko tayari kukupokea, kama uko tayari kumpokea.

Sasa inua mikono yako na uombe pamoja nami.

85 Bwana Mungu, jalia makuhani wote washikilie madhabahu. Jalia watu walie. Jalia ile Nguzo ya Moto na ile Nguzo ya Wingu iingie ndani ya watu leo na kuwatia akili, Bwana, kwenye utambuzi wa Uwepo wa Mungu aliye hai na mwenye nguvu. Tujalie, Bwana. Wapokee. Ninaomba maombi haya kwa ajili ya kila mmoja wao, katika Jina la Yesu Kristo.

Jaza kila mmoja na Roho Mtakatifu, ambaye hana Roho Mtakatifu. Bwana, jalia uamsho wa kampeni hii, mkutano huu, utokee sasa hivi katika kumwagwa kwa nguvu kuu za Roho Mtakatifu. Jalia wagonjwa waponywe, vipofu waone, viwete watembee. Jalia udhihirisho wa Mungu aliye hai uletwe kwenye uwepo wa watu, kama ilivyokuwa alasiri ya leo, na jalia watu walipokee. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba.

Inueni mikono yenu sasa na mumpe sifa, na mpokee mlichoomba.

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7